Mtu Anayejiepusha Na Uso Wa Bwana

Na tuviinamishe vichwa vyetu. Mungu mpenzi, tuna furaha alasiri ya leo kwa majaliwa haya tuliyo nayo ya kukusanyika pamoja mara nyingine. Na Wewe peke Yako, Bwana, unajua jinsi mioyo yetu imekuwa na shauku kwa ajili ya saa hii wakati ambapo tunaweza kusimama mbele ya watu Wako tena hapa, na kuuleta Ujumbe huu ambao tunaona kabisa kwamba ni wa lazima sana katika saa hii. Umetugawia siku hizi chache sasa, nasi tunaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba mkono Wako wa rehema utakuwa juu yetu, kutuongoza na kutuelekeza. Na utupe mambo yale tunayohitaji, Bwana, kwa maana mioyo yetu ina shauku sana ya kukujua vizuri zaidi.

2 Tunaona mashamba makubwa ya mavuno, meupe, yameiva, na tunajua nafaka iko tayari sasa kwa ajili ya ule wakati mkuu wa kupura. Mungu mpenzi, tunaomba ya kwamba utayafungua uyaondoe makapi yanayotuzunguka, ujalie tukae katika Uwepo wa Mwana sasa, siku hizi chache zijazo, tupate kuiva kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

3 Bariki kila wimbo utakaoimbwa. Bariki kila ombi, na ujibu kila moja litakaloombwa, Bwana. Waokoe wote waliopotea. Waite warudi katika nyumba ya Mungu aliye hai, na katika ushirika, wale ambao wamepotea.

4 Tunaomba, Mungu, ya kwamba utamponya kila mgonjwa anayekuja chini ya dari yetu. Tujalie, Bwana. Naomba kusiwe na mtu aliye mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa mikutano hii.

5 Pia, Mungu Mpenzi, tena kwa ajili yetu, sisi ambao tunadai katika saa hii kuwa Kanisa, Walioitwa watoke, wale kote ulimwenguni ambao wametoka katika Babeli wawe washiriki wa ushirika huu wa ajabu katika siku hii ya mwisho, tunaomba Mungu ya kwamba Wewe utaibariki mioyo yetu kwa njia kama hiyo. Sisi tuna njaa kweli, Bwana, na tumejiweka tupu na mambo yote ya ulimwengu, tuyajuayo. Bwana, tumeweka kando kila mzigo unaotuzinga kwa upesi, na sasa na tupige mbio kwa subira katika mashindano haya, ambayo yamewekwa mbele yetu. Tujalie, Baba. Na jalia tuwe Wakristo waliokomaa zaidi, wenye nguvu zaidi na wema zaidi, mwishoni mwa ibada hii, kuliko tulivyokuwa tulipoingia. Mungu na apate sifa zote, kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

6 Nafikiri haya ni majaliwa mazuri, usiku huu, ambayo nimengojea kwa muda fulani. Juzijuzi nilikuwa nikimwambia

mke wangu, nikasema, “Ninashikwa na wasiwasi sana, nikingojea kwenda kwenye Maskani.” Nina ninino tu . . . Nina marafiki wengine, bila shaka, ninao, kote ulimwenguni, bali kuna kitu fulani ama cho chote kile juu ya Maskani haya hapa.

Nilitolewa kwenye vumbi hili hapa, wakati Mungu aliponipa uhai hapa duniani; nami nafikiri, kama Yeye akikawia, nitazikwa hapa mahali fulani. Yeye atakapokuja, atanikuta hapa mahali fulani.

7 Lakini, yaonekana kwamba, kuna kitu, ninapoanza kufikiria juu ya Jeffersonville. Hivi majuzi nilishikwa na ukiwa sana; nikamwambia mke wangu, nikasema, “Nina waza kwetu, nami sijui kwa nini ninawaza kwetu, isipokuwa iwe kwamba hao watu wananiombea.” Nikasema, “Vema, nita- . . . Jambo nijualo tu kufanya ni kurudi na kuwa na siku chache za mikutano, tuone kama hatuwezi kupata kitu kutoka kwa Bwana, labda anataka sisi tujue jambo fulani.”

Na somo kuu lililo muhimu sana tulilo nalo mbele zetu ni *Ndoa Na Talaka*. Na kama kuna swali, hapana budi kuwe na jibu. Hapawezi kuwa na swali pasipokuwa na jibu. Hata liwe ni nini, hapana budi pawe na jibu. Na kama Bwana akipenda, nataka kujaribu kuzungumzia juu ya jambo hilo, Jumapili asubuhi.

8 Halafu, kesho usiku, nafikiri tunapaswa kuwa hapa kwenye . . . Shule hiyo inaitwaje? [Ndugu Neville anasema, “Parkview.”—Mh.] Ukumbi wa Parkview. Ati nini, bwana? [“Parkview Junior High.”] Parkview Junior High. Ni wangapi wanajua mahali ilipo? Vema, nafikiri watakuwa na kibao cha kuwaelekeza kule, sivyo, Ndugu Neville? [“Naam.”] Itakuwa . . . Iko tu juu hapa—yapata robo tatu za maili, kutakuweko na kibao cha kuwaelekeza. Unageuka unarudi, unaiacha barabara. Ni jengo zuri, lililoinuka. Lina mahali ambapo unaweza kuwekelea mkono wako, na kuandika yale unayotaka kuandika, na—na—na kadhalika. Nami nina hakika mtalifurahia kidogo zaidi kuliko vile mtakavyokuwa, mmesongamana kwa namna fulani katika mikutano hapa kwenye—kwenye Maskani. Kutakuwa na nafasi kubwa, nafasi kubwa ya kuegesha magari.

9 Sasa, nafikiri walikuwa na utaratibu mdogo uliotubidi kuahidi kuufuata, ambao ulikuwa, tusije mahali pale mpaka saa kumi na mbili u nusu. [Ndugu Neville anasema, “Wasije mpaka saa kumi na moja u nusu; wasiwe kule kabla ya saa kumi na moja u nusu.”—Mh.] Na ni saa ngapi . . . [“Milango itafunguliwa thenashara u nusu.”] Naamini ni wazo zuri kwetu kufika pale saa kumi na mbili u nusu.

Naam, wana jumba lingine la mikutano hapa mjini linalokaa watu elfu sita. Tukiwa wazuri sana katika hili, huenda wakaturuhusu kuchukua hilo lingine wakati mwingine kwa ajili ya mkutano mkubwa, labda wakati mwingine kwenye msimu huu wa kiangazi nitakaporudi kutoka nchi za ng’ambo.

10 Na kwa hiyo nafikiri tunaweza kukaa mpaka . . . Tunaweza kukaa wangapi kule? [Ndugu Neville anasema, "Tunaweza kukaa kama watu elfu nne."—Mh.] Elfu nne. Kwa hiyo, mnaona, tutakuwa na nafasi kubwa sana. Hakutakuwa na kuharakisha. Na kwa hiyo fikeni mnamo saa kumi na mbili u nusu. Basi kila mtu anaweza kuja kwa wakati unaofaa, kila mtu pamoja, nami nina hakika m-—mtapata viti vizuri. Na pameinuka namna *hii,* na—na mahali hapa ambapo unaweza kuandika na kunakili maneno machache, na kadhalika. Na hiyo itaanza, Bwana akipenda . . .

11 Nafikiri sasa, usiku huu, huu ukiwa ni mkutano wa maombi ya Jumatano usiku, tuna . . . Mahali hapa karibu pamejaa kabisa, kwa hiyo nafikiri afadhali tuanze kesho usiku. Tulipakodisha tu tukiwa na matumaini ya kwamba labda, kama tukiwa wa kutosha hapa na kujaa kabisa, tungeweza kwenda kule. Bali naamini ni . . . ingekuwa ni vizuri zaidi kwenda kule, sivyo, Ndugu Neville, kwenda kule kesho usiku? Na ni wangapi wanaofikiri hilo lingekuwa ni wazo zuri? Ndipo mnaweza kupata nafasi kubwa ka—kabisa. Ta—tayari umekodiwa; umegharimiwa na ndugu fulani hapa kanisani. Unatugharimu dola hamsini usiku mmoja, ambayo ni ninino sana, sana . . . Laiti ningalipata kama huo kila mahali, ambao ungekaa kiasi hicho cha watu kwa dola hamsini kwa usiku, jumba jipya kabisa, jukwaa zuri. Na, bali tuna . . .

12 Bila shaka, tutachukua sadaka, nafikiri. Na hatutaki hao watu wagharimie hilo wao wenyewe; tutagharimia . . . tutawarudishia. Lakini tutakapopata matumizi yetu na kadhalika, vema, basi, bila shaka, tunaweza kuacha kuchukua sadaka. Hatu- . . .

13 Kama kuna mgeni ye yote pamoja nasi, tumetoa uamuzi huo, hatutaomba kamwe, kushawishi, kuwasukuma watu kwa ajili ya pesa. Sisi huzungusha sahani ya matoleo, jambo ambalo tu ni . . . Hilo ni tendo la kidini. Nimelijaribu, mara nyingi, hata kutozungusha sahani ya matoleo, hata kidogo, bali haifaulu. Mnaona? Kwa sababu, kutoa ni sehemu ya dini yetu. Ni moja ya jukumu letu. Hata kama ni hela moja tu, ama cho chote kile, ama peni, yote ni . . .

14 Kwa hiyo unakumbuka, Yesu alimwona mjane akipita, siku moja, mahali ambapo matajiri walikuwa wakitoa kwenye hazina sehemu kubwa ya hazina zao. Basi huyo mjane akapita, labda baadhi ya watoto wadogo wenye njaa wakitembea karibu naye, naye akatoa kila kitu alichokuwa nacho, peni tatu. Ndipo Yesu akasema, "Ni nani aliyetoa zaidi kuliko wote?"

15 Naam, kama ningalikuwa nimesimama pale, ningalisema, "Usifanye hivyo, dada. Sisi—sisi, angalia, tuna pesa nyingi sana." Bali Yeye hakumkataza kamwe. Mnaona? Alijua alikuwa na kitu kikubwa zaidi kwa ajili yake siku za usoni. Kwa hiyo, mnaona,

hata hivyo, yeye alikuwa na makao Utukufuni, alikokuwa anaelekea. Naye kamwe hakumkataza. Alimwacha atoe peni zake tatu, kwa maana yeye alitaka kufanya hivyo. Na ilimbidi kutaka kufanya jambo hilo; huku ana watoto, na ni mjane, na ana peni tatu tu za matumizi yake. Yeye, ilimbidi mwanamke atake kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, mnaona, wakati watu wanataka kutoa, huna budi kuwapa nafasi ya kutoa.

16 Lakini nafikiri juu ya hawa wanaosimama, huku watu wakisema, "Ni nani atakayetoa dola hamsini? Ni nani atakayetoa dola ishirini?" Nafikiri jambo hilo linaidhuru akili ya—yako. Na—nafikiri ya kwamba watu wanatambua ya kwamba inahitaji pesa ku—kuendeleza m—mkutano. Nami kamwe nisingewaruhusu kufanya jambo hilo, mameneja wangu. Nikasema, "Wakati wo wote itakapowalazimu kufanya hivyo, basi wakati wangu wa kurudi kwenye Maskani umewadia. Kwa hiyo, haitatulazimu kufanya hivyo." Bali na—nafikiri inatubidi kuzungusha sahani ya sadaka, ku—kusudi tuifanye ibada kamilifu ya kidini.

17 Na kwa hiyo labda watazungusha sahani ndogo ya sadaka kila usiku, waseme kitu kama, "Vema, tutachukua sadaka sasa." Nao watazungusha sahani ya sadaka, na huo utakuwa—huo utakuwa ndio mwisho wa jambo hilo.

18 Na kila usiku, Bwana akipenda, nafikiri Bwana ameweka moyoni mwangu Ujumbe dhahiri sana kwa ajili ya Kanisa. Nimekuwa nikiomba kwa siku nyingi. Nami sitaingilia jambo hilo, kwa maana tukio kubwa sana lilitukia hivi majuzi ambalo kweli lilikuwa kubwa. Nami nina hamu ya kuwaambia jambo hilo. Na sasa, somo muhimu, nafikiri, ambalo wengi wao, Billy alisema, wamekuwa wakipigia simu, lilikuwa juu ya *Ndoa Na Talaka*. Ambalo, ni somo mu—muhimu sana, na si—sijui jinsi ya kuliendea. Nami nilipanda nikaenda kuomba juu yake, ndipo Bwana akakutana nami. Nami najua ya kwamba mimi, kwa . . . sina, bali Mungu amenipa; ninalo sasa. Mungu amenipa jibu sahihi, mnaona, mnaona, nami na—najua ya kwamba ni kweli.

19 Na kwa hiyo bado sijui hasa, labda, Jumapili huenda nikawaomba dada zetu wasiuhudhurie huo mkutano, wao wenyewe, lakini si—sijui. Itategemea kama wanawake walioolewa wanataka kuja pamoja na waume wao. Kuna—kuna mambo muhimu sana kweli yanayopaswa kusemwa, ukweli wake, na ni jinsi gani. Na kwa hiyo tunataka kulielezea vizuri kabisa, ya BWANA ASEMA HIVI, ndipo mmelipata basi. Mnajua tu Kweli ni nini basi. Nami ninaamini atafanya hivyo.

20 Na, sasa, nilikuwa huku juu kwenye ule mkahawa hivi majuzi, nikila, huku—huku Jerry na hao wengine wote wakiwatafuta nyinyi nyote. Walisema, kasema, "Vema, sisi . . ." Wengine, mmoja wa hao wavulana alikuwa ameamka, kasema, jamaa huyu alisema, "Nitafanikiwa vizuri sana juma hili,"

kasema, "wao wana . . . Ama, majuma haya machache yajayo." Kasema, "Wao wana mkutano hapa, wa mpira wa vikapu, ama kitu kama hicho." Kasema, ndipo kasema, "Branham yuko huko chini, atakuwa na mkutano." Akasema, "Nitawalisha watu wengi sana." Kule kwenye Ranch House, moja ya mahali hapo kule juu. Nao walikuwa . . . imekuwa nzuri sana.

21 Nami nawafurahia nyinyi nyote, kwa maana bila shaka waliwasifu na kusema mambo mzuri juu yenu.

22 Meneja juu kule kwenye Ranchi House alikutana nami hivi majuzi asubuhi. Nilifika kama saa nane u nusu, kutoka Arizona. Naye akasema, "Vema, Ndugu Branham," kasema, "nasikia utakuwa na mkutano mwingine." Kasema, "Nilipata msaada zaidi," akasema. Kisha akasema, "Basi nataka kusema jambo moja, ya kwamba watu hao wanaotoka kule chini," kasema, "hao kweli ni watu wazuri." Naam, jambo hilo lilinifanya nijisikie vizuri kweli juu yenu, mnaona.

Maana, hata hivyo, kwa namna fulani najisikia ninyi ni wana-mbuzi wangu, nami na—na . . . ama, watoto, hasa. Na kwa hiyo mimi . . . Wana-mbuzi linahusu mbuzi, nanyi si mbuzi. Ninyi ni wana-kondoo wangu. Mwaonaje? Ninyi ni wana-kondoo wa Bwana ambao ameniruhusu kuwalisha. Nami natumaini ya kwamba ita—ita . . . ya kwamba Yeye ataniruhusu nifanye hivyo. Tunaenda zetu barabarani.

23 Na kuhusu hii *Ndoa Na Talaka*, nimetaka kuzungumzia habari zake tangu wakati wa zile Muhuri Saba. Mwajua, zile si- . . . Siri zote zilipaswa kujulikana katika hizo, kufunguliwa kwa hizo Muhuri Saba, siri zote za Biblia. Nami ninafikiri sasa, kwa namna fulani ninakuwa mzee, na—nafikiri mimi . . . nilifikiri afadhali niyanase kwa kanda, ili kwamba kama jambo fulani likinipata, basi Kanisa linaweza kushangaa, "Sijui alikuwa anawaza nini? Yeye angesema nini?" Na mambo hayo yote yanayoonekana magumu sana; nafikiri, kwa msaada wa Bwana, nitajaribu kuyaleta kwenu. Ndipo basi—basi kama kitu fulani kikitukia, na kama ikitokea kwamba nitaaga dunia kabla ya kuja Kwake, mta—mtakuwa na kumbukumbu yake.

24 Nafikiri tuna vitabu vipya ambavyo vimetolewa. Namwona Dada Vayle; sijui kama daktari yuko hapa ama hayuko. Yuko hapa, Dada Vayle? Huenda ikawa yuko mkutanoni. Simuoni. Lakini, loo, ndiyo, huko nyuma kabisa. Naye Ndugu Vayle ameandika kitabu, na ni . . . Nilifikiri, nafikiri walisema leo, viwili. Ndugu Vayle, hiyo ni kweli, una vitabu viwili hapa sasa? Vitabu viwili. Sasa, sijui, mimi . . . Ninavyoelewa mimi, ya kwamba kila mtu atapata nakala. Kwa hiyo mimi . . . Kama ninyi . . . Hivyo ndivyo ninavyoelewa. Huenda nimekosea katika jambo hilo.

25 Tena *Nyakati Saba Za Kanisa* kimekwisha (sivyo, Ndugu Vayle?) na sasa kinachapishwa. Nami najua mtapenda kuvipata,

maana vinajibu maswali mengi sana ambayo yamekuwa mioyoni mwenu. Kisha baada ya hayo, vema, tutajaribu kuziandika zile *Muhuri Saba* zilizofunguliwa, mwajua, katika kitabu, ili kwamba kila mtu apate kusoma katika hali ambayo wao—ambayo wao wanataka, wanayoweza kuelewa na kusoma. Nafikiri kitakapoandikwa, kama kita-. . .

26 Kwanza, tulikitoa moja kwa moja kutoka kwenye kanda, jinsi kilivyokuwa kimeandikwa ama kunenwa. Mnajua, unaweza kuhubiri somo, ni jambo moja, kisha kuandika kitabu ni jambo lingine. Mnaona, kama vile ningegusia somo fulani, kama vile ningewaambia, mngeelewa, ningesema, "Naam, ule uzao wa nyoka," mnaona.

Vema, sasa, mwenye kukisoma hicho kitabu, kama ukiondoa jambo hilo, angeshangaa, "Uzao wa nyoka ni nini?" Mnaona? Nao hawangejua. Kama jambo hilo likitokea kwenda mahali kama Princeton ama mahali fulani, nao wange—wangefikiri sisi ni watu wasio na akili.

Kwa hiyo nilimwomba Ndugu Vayle kwa namna fulani anisaidie katika jambo hili na kushikilia wazo lile lile, na kukipa sarufi. Nami nina hakika sarufi yangu wao wange-. . . Ingekuwa fumbo kwao, bila shaka. Kwa hiyo huyo. . . Ndugu Vayle ni hodari sana katika jambo hilo, kwa hiyo yeye ni . . .

27 Halafu, katika jambo hilo, nafikiri ndugu yetu mpendwa hapana budi alipata kuvuviwa kudogo zaidi, kwa namna fulani, naye alisema ataandika vitabu kadha vyake binafsi, kutoka kwa hivyo, namna hiyo. Na kwa hiyo aliandika kimoja kinachoitwa, naamini, *Nabii Wa Karne Ya Ishirini*, na kingine, *Kanisa La Laodikia*, naamini, ama kitu kama hicho.

28 Naye Billy aliniambia usiku huu ya kwamba naamini maelfu ya hivyo vimewasili leo; mtu fulani alivileta kutoka Texas. Na kwa hiyo, hivyo, vitakuwa hapa. Nao watatangaza jambo hilo, nafikiri, vyo vyote vile. Nafikiri vimedhaminiwa. Sina uhakika. Na kama vimedhaminiwa, vitatolewa kwenu, mnaona, pia, bure. Nasi tunatumainia mtafurahia jambo hilo. Na kama mkilifurahia, mpe Ndugu Vayle mkono pale na kumwambia jinsi mnavyofurahia jambo hilo. Sijakisoma, mimi mwenyewe. Kama ningevisoma, huenda nikabadilisha nia yangu juu yake, kwa hiyo nitajaribu kuvisoma juma hili wakati nina nafasi, kama nikiweza.

29 Sasa kwa kuwa ni Jumatano usiku, mkutano wetu unaanza rasmi kesho usiku. Bali nafikiri, kwa maana niko hapa kati yenu, ni—ni—nisingekaa kule nyumbani na—na kujua kwamba ninyi nyote mlikuwa hapa. Mimi. . . Kama tu, mwajua, kama vile baadhi ya watu wenu wanakuja, mwajua, nanyi mnashuka manaenda mbio kwenye mwisho wa njia kuwalaki, mwajua. Nami—nami nilifikiri ningeshuka nije mbio na—na

kuwakaribisha Jeffersonville. Na kwa hiyo juma hili la mwisho mimi karibu ni-. . .

La, samahani, imekuwa yapata majuma matatu yaliyopita, nilikuja nyumbani. Nimekuwa kule nje nikijaribu ku-. . . Nimekuwa nikifanya mikutano kupitia Arizona kule, nami nikarudi kusudi nijaribu kupumzika. Basi nikaondoka nikafanya safari ya kuwinda, ndipo—ndipo nikavunja rekodi ya mkoa wa Arizona ya kuwinda simba. Nilimfukuza maili ishirini msituni kumpata.

30 Halafu basi kufikiria, hata hivyo, ya kwamba kamwe sikufikiria nilipokuwa mvulana mdogo. . . Kuonyesha tu jinsi mambo haya yanavyotokea, mahali padogo ambapo Bwana ametupa kule, kwa ile miezi tuliyokuwa kule, na shule kwa ajili ya watoto.

Nilikuwa mvulana mdogo. Nafikiri Jimmy Poole yuko hapa usiku huu, labda baba yake yuko hapa, Jim mkubwa. Tulisoma pamoja, nami nakumbuka nikiketi pale, kama maskini mtoto mdogo aliyevalia matambaa, na viatu, nimevaa viatu vya mchezo wa tufe, huku vidole vinatokeza; ninamwomba mmoja kipande cha karatasi, na mwingine penseli.

31 Nilizoea kuandika mashairi. Na Bibi Woods, hapa, aliniomba kukariri hayo alasiri ya leo kwenye kanda, juu ya Ford yangu, mwajua, na ni—ni zuri. Sasa, yeye alisema, "Vema, unapaswa kuyatuma hayo kwa Bw. Ford."

Nikasema, "Kuna ukweli mwingi sana, naamini," kuhusu kutatarika upande wa mbele, na kukereza katika gia, na fumbo la Kichina ndilo gia ya kuiendesha. Lakini mimi. . . Ni—ni. . . Bali daima nilisema, jambo tu nililopaswa kufanya ni kuhesabu tairi nne, na kuitikisa vya kutosha kuifanya ianze kwenda kisha ninaingia. Nilisema, "Ilikuwa nzuri wakati nilipoanza kupanda kilimani nayo, inaenda ikijikokota pole pole sana, ikisema, 'Nafikiri naweza, nafikiri naweza, nafikiri naweza.' Kisha inaanza, upande wa pili, ikisema, 'Nilifikiri ningeweza, nilifikiri ningeweza.'" Mnaona?

Hivyo ndivyo tunavyojikokota kwenye kilima hiki, kama *Safari Ya Msafiri*. Kwa hiyo sisi. . .

32 Nilikuwa nimeandika shairi dogo, kitu kama hiki. Nami nikasema. . . Naam, waza tu, nilikuwa na kama tu umri wa miaka kumi na miwili. Nami nikisimama pale juu, hivi majuzi, nikiangalia kule kwenye magenge yale; nami nikifikiria simba yule atakuwa amekaa papa hapa katika chumba hiki changu cha faragha akikitazama dirishani, kwenye dirisha la kioo. Nilikuwa nikiwazia juu ya shairi dogo. Niliondoka nikaenda nikalichukua, kitu kama hiki. Wazia tu jinsi Mungu. . .

33 Mnaamini Mungu yuko katika uvuvio wote? [Kusanyiko linasema, "Amina.—Mh.] Mungu hana budi kuandika wimbo. Mnaamini Mungu yuko katika nyimbo? ["Amina."]

Yesu alisema hivyo. Alirejea kwa Daudi, "Hamjui aliyosema Daudi katika Zaburi? Mwajua, haja-. . . "

34 Angalia kwenye kule kusulubiwa kwenyewe. Daudi alikuimba, katika Zaburi 22, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, Mbona umeniacha? Mifupa yangu yote inanikodolea macho. Wamenizua mikono na miguu." Mnajua, na huo ulikuwa wimbo. Zaburi ni—ni wimbo.

35 Na katika mashairi haya, angalieni tu jinsi ulivyotimia. Nikiketi pale, maskini mtoto mdogo na kipande cha karatasi cha kuazima, nikasema:

Nina upweke, loo, nina upweke sana kwa ajili ya ile kusini-mashariki ya mbali,
Ambako vivuli hushuka chini sana juu ya kilele cha mlima.
Naweza kumwona mbwa mwitu wa mbugani akiotea karibu na ukungu wa zambarau;
Naweza kumsikia lobo akipiga makelele mahali wenye pembe ndefu wanakulia majani.
Na mahali fulani juu ya magenge naweza kumsikia simba akilia,
Kule mbali kwenye Milima ya Catalina mpakani mwa Arizona.

36 Miaka arobaini baadaye, ninaketi pale pale kwenye yale magenge, yule simba akiniangalia moja kwa moja usoni.

Ee Mungu, kuna Nchi kule ng'ambo ya mto mahali fulani, marafiki. Ni kwamba tu haina budi kuweko. Mnaona? Kuna—kuna kuzungumzia mengi sana juu yake. Mambo haya yote si hadithi za kubuni; ni . . . Ni halisi. Ni dhahiri. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo, kuwa pamoja na watu hawa ambao natarajia kuishi nao kule Ng'ambo, ambako hakutakuwa na maradhi tena, ama mauti, ama matengano. Na kusafiri hakutakuwa kitu kwetu wakati huo.

37 Sasa, nafikiri hakuna mkutano ulio kamili bila ya kusoma Neno na kuwa na ninino kidogo . . .

Ndugu Neville, ndiyo kwanza nije hapa. Billy alisema ulitaka nizungumze. Hiyo ilikuwa kweli, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Amina. Naam. Bila shaka."—Mh.] Naam, huenda nikachukuliwa kwa urahisi sana, bali ni—nilijisikia tu vizuri sana kuhusu jambo hilo. ["Vema, amina! Bila shaka!"]

Kwa hiyo, sasa, ninyi ambao mna nyimbo na kadhalika, mwoneni Ndugu Neville wakati mtakapoimba, ndipo muimbe, kule. Basi iweni na kama nusu saa ya utangulizi, ndipo nasi tuingilie Jumbe hizi zenye kilindi sana na tuone kile tunachoweza kuona atakachofanya Bwana. Nami natumaini tu . . .

38 Na—naamini tuna Kweli. Nimeridhika na jambo hilo. Nami naamini ya kwamba ngano imeninino, kabisa, makapi yanaondoka kwake. Mnajua. Pia, mnaona, naweza kutoa utangulizi mdogo hapa juu ya jambo hilo, usiku wa kesho, mnaona, jinsi makapi yanavyojiondoa kwenye ngano. Bali ngano haina budi kukaa katika Uwepo wa Mwana, ipate kuiva. Na hilo ndilo kusudi letu la kuwa hapa, rafiki, kukaa katika Uwepo wa Mwana hata kundi letu dogo la watu hapa, hata litakapoiva sana kwa ajili ya Kristo, liwe mkate kwenye meza Yake. Hivyo ndivyo ninalitaka lifanye.

39 Na sasa kabla hatujalikaribia Neno, baada ya kukariri mashairi, na kadhalika, na tuombe tena. Ndipo tutachukua somo.

40 Mpendwa Yesu, tusaidie usiku wa leo, katika maneno haya machache, tunapokungoja Wewe. Nasi tunaomba ya kwamba neema Yako na rehema itakuwa pamoja nasi, Bwana. Na ifanye mioyo yetu kuwa miororo; ondoa makapi yote, miiba, michongoma, naomba kwamba jua la Mungu lenye baraka liliangukie Neno, Bwana. Pia naomba kwamba tuwe na mkutano mkubwa sana hata hapatakuwepo na mtu ye yote ambaye hajaokoka miongoni mwetu, watoto wote watakuwa katika Ufalme wa Mungu. Wale wasio na ubatizo wa Roho, naomba kwamba waupokee, Baba. Naomba kwamba siri zote kuu tunazopaswa kujua kwenye wakati huu, Bwana, zifunuliwe kwetu; nasi tutaona urahisi wa Mungu, ili kwamba tujue jinsi ya kuenenda na kutenda, tukijisahihisha na kuvitiisha viungo vya miili yetu kwa Neno, kusudi tujue jinsi ya kuishi katika siku hizi wakati kuja kwa Bwana Yesu kunapokaribia.

41 Ninaposoma Neno Lako usiku huu, Bwana, naweza, kwa elimu haba, naweza kusoma baadhi ya maneno, na labda nitamke vibaya mengine. Bali, Bwana Mungu, Wewe peke Yako Ndiwe unayeweza kutoa yaliyomo mle. Wewe Ndiwe tu unayeweza kufanya hivyo. Ha—hakuna mwanadamu anayeweza kufanya hivyo kamwe; iko mikononi Mwako, Bwana. Kwa hiyo tupe sisi, kila usiku, hayo mambo ambayo yamefichwa katika Neno Lako, ili kwamba tuweze kuwa Wakristo bora na kuishi kulingana na wakati tunaoishi, kama mifano ya Ukristo. Tunaomba katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

42 Sasa, wengi wenu, katika Biblia zenu, nawatakeni mfungue katika Kitabu cha Yona. Ni. . .Daima tunazungumzia habari za Yona kwamba alikuwa amerudi nyuma na kadhalika. Mimi daima nimemtetea Yona. Siamini ya kwamba Yona alikuwa amerudi nyuma. Si—siamini jambo hilo. Naamini ni kwamba tu. . .Wakati mwingine tunaitumia, tunasema, “Yeye ni Yona.” Bali kama sisi. . .Tayari nimezungumzia jambo hilo, kwa njia nyingine, katika kuwaambia jinsi nilifikiria, Yona, yaliyotukia.

Basi neno la BWANA lilimjia Yona, mwana wa Amitai, kusema,

Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukapige kelele juu yake; kwa maana uovu wao umepanda juu mbele zangu.

Lakini Yona akaondoka akakimbia Tarshishi, apate kujiepusha na uso wa Bwana; akatelemka hata Yafa, akaona merikebu inayokwenda Tarshishi; basi, akatoa nauli, akapanda merikebuni, aende pamoja nao Tarshishi, ajiepushe na uso wa BWANA.

43 Huo si ni mwisho wa kusikitisha? *Mtu Anayejiepusha Na Uso Wa Bwana*, na hilo ndilo somo langu.

44 Sasa, kwanza tunataka kufikiria jambo hili. Yona alikuwa. . .Sababu, sababu iliyo muhimu, ambayo naamini yeye alifanya jambo hilo kubwa hapa, ilikuwa kwamba Yona alikuwa Myahudi. Naye aliagizwa kwenda katika jiji la Mataifa, akapige kelele juu yake; akifikiri ya kwamba hawangempokea. Kwa maana, Mataifa wangefikiri, "Huyu Myahudi ana uhusiano gani nasi?" Bali, unaona, jambo lingine, inatupa jambo kubwa hapa kuona, ya kwamba Mungu si Mungu wa Wayahudi tu, bali pia ni Mungu wa Mataifa. Yeye ni Mungu wa watu wote.

45 Yeye aliwachagua tu Wayahudi. Wayahudi waliitwa watu wa Mungu waliochaguliwa. Wao walichaguliwa kwa kusudi fulani. Na kusudi hilo lilikuwa, kuwapa torati, nao hawangeweza kuitimiza. Naye alionyesha tu, kwa watu hao, ya kwamba torati haingeweza kutimizwa, na kwamba Yeye alikuwa Mu—Mu—Mungu mwenye haki. Nayo torati ilidai haki, bali hakukuwa na neema katika torati, kumfungua mtu. Hakuna hukumu iliyolipiwa na torati, bali ilihitaji neema kuilipia hiyo hukumu, ama mahali torati ilituingiza.

46 Naye Yona hapa aliitwa, kama huyu, mmoja wa manabii wadogo wa Biblia, ashuke aende kwenye jiji hili.

Na hapa tunaona mfano wetu sote. Kila mmoja wetu, daima tunajiepusha na kitu fulani. Tunajiepusha na shida. Tunajiepusha na majukumu. Sisi, sote tumezoea kufanya hivyo. Sisi, tuna, tumezoea sana kukimbia kuliko tulivyozoea kulikabili jambo fulani. Mnaona, sisi tu. . .tuna—tuna—tunajikuta tukikimbia.

Wakati mwingine tunajikuta tumezoea kujiepusha na kazi. Hatutaki, hatutaki kufanya kazi. Watu wengine hufikiri tu wanaweza kupata riziki bila ya kufanya kazi. Bali, nafikiri, Sulemani ndiye aliyesema ya kwamba tungeweza kupata jawabu hapa, kwa kumtazama chungu.

47 Unajua, chungu mdogo, wananiambia kama huyo (kila) chungu hafanyi kazi na kuweka akiba, huyo chungu hatakula

katika msimu huo wa kipupwe, basi. Kwa hiyo, kila mtu hana budi ku—kufanya kazi.

48 Tuna mambo mengi sana yatupasayo kufanya, majukumu mengi sana yanayotupasa kukabiliana nayo. Kila mtu hana budi kukabiliwa na jukumu fulani.

49 Wakati wewe—wewe unapofikia ku—kumchagua mke wako, kuoa, ama kuchagua mume wako, hu—huna budi kukabiliwa na jukumu fulani. Kisha huna budi kukumbuka . . . Labda unajenga nyumba; ni nyumba nzuri na ya kupendeza. Kisha, kumbuka, kama mwanamke aliyeolewa, huna budi kufikiria juu ya jukumu la kuwalea watoto. Na huna budi kufikiria juu ya hizo kuta nzuri na za kuvutia zitakuwa na alama za mikono midogo michafu kila mahali. Kisha una jukumu la kuwaelimisha watoto wako. Una jukumu la kuwavika nguo na kuwalisha.

50 Kila kitu ni jukumu. Na ni rahisi sana, wakati tunakabiliwa na majukumu, kuyaepa. Nasi tunaona ya kwamba ndoa ni jukumu, na kila hali.

51 Hata, mara nyingi, tunaona . . . Ni vigumu kusema jambo hili, bali ni kweli, ya kwamba wahudumu, mara nyingi, wanaepa jukumu la kutetea Neno la kweli la Mungu wanapokabiliwa Nalo. Wao wanaepa jukumu hilo. Wakati Neno la Kweli la Mungu linapoletwa uso kwa uso mbele ya wanadamu, tuna . . . tumezoea kuliepa kwa dhati kabisa.

52 Ndio kwanza nimalize kuzungumza na maskini mpwangu pale. Yeye ni Mkatoliki, naye . . . Nami nilimbatiza mvulana huyo, katika Jina la Yesu Kristo, hapa miaka michache iliyopoita, naye akaambatana na maskini msichana mmoja ndipo akageuka akawa Mkatoliki. Nami niliushika mkono wa mama yake alipokuwa akifa kule. Yeye akaniambia, maneno ya mwisho, "Mwangalie Melvin." Naye amekuwa akiota tu ndoto. Yeye hawezi tu . . . Kila, kila siku, juma la mwisho, amekuwa akiota ndoto. Kasema, "Ningeingia kanisani mwako, Mjomba Bill, nawe ulikuwa umesimama pale ukihubiri. Ningekuja mbio, nikaanza kutubu. Kisha ningeamka." Yeye akasema, "Ni—nimekosea."

Nikasema, "Melvin, huhitaji tafsiri yo yote juu ya jambo hilo. Mahali pako ni kule chini ambako wewe ni mshiriki wake." Hiyo ni kweli. Mnaona?

53 Bali kukabili majukumu, mara kwa mara tunapigwa vita sana, kufanya jambo hilo. Kama baba, kulikabili jukumu, mpige mtoto wako. Hao jamaa wadogo, hutaki kufanya hivyo. Bali kama baba ama mama, huna budi kulikabili jukumu la kumlea mtoto huyo, kwa maana Biblia ilisema, "Usipotumia fimbo, utamharibu mwanao." Na jambo hilo lingali linafaa mbele ya uso wa kila mwanasaikolojia aliyeko ulimwenguni. Hiyo ingali ni Kweli ya Mungu. Kama jambo hilo lilitekelezwa zaidi, tusingalikuwa na hatia nyingi sana za watoto na kadhalika, na

upotovu tulio nao ulimwenguni leo. Bali ule usia mwema wa kale wa nyumbani umevunjwa, zamani za kale, nao wanawaacha watoto wafanye watakayo.

54 Bali kama nilivyosema, wahudumu, watakabiliana uso kwa uso na ile Kweli, kisha waiache waende zao. Mnaona, wao—wao wana ninino tu. . .Inaonekana kama kwamba kuna kitu ambacho wao—wao hawataki kukikabili.

55 Mara nyingi watu wamenijia, wakasema, "Najua jambo hilo ni kweli, Ndugu Branham, lakini kama ningelifanya hivyo, wao wangenifukuza kanisani." Unajali nini? Kama hutafanya hivyo, wao watakufukuza, Kule juu. Kwa hiyo huna budi kufukuzwa, mahali fulani, unaona. Kwa hiyo afadhali ukabiliane nalo, badala ya kulitoroka na kusema, "Vema, nitaondoka niende *huku*. Sitarudi." Rudi, kweli, sikiza mengi zaidi Yake.

Yachunguze Maandiko. Yesu alisema, "Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani Yake, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Bali tunaona ya kwamba watu hawatakabiliana na jambo hilo.

56 Wakiletwa kwenye, katika Uwepo wa Mungu, na kuona wakati Mungu alifanya ahadi, na Mungu anawajibika kutimiza ahadi hiyo. Na wakati anapotimiza hiyo ahadi, ndipo watu wanaogopa kukabiliana na jukumu la kutekeleza ujumbe wa Wakati. Tunaona jambo hilo kila mahali.

57 Na nyinyi Waluteri je? Ni Waluteri wangapi waliogopa, watu walioogopa kuukabili Ukweli wa Luther alipojitokeza na kuhesabiwa haki? Angalieni ulichowagharimu, labda maisha yako mwenyewe, kujitokeza na kumkiri Yesu Kristo na—na kuwa M—Mluteri.

58 Jiangalieni enyi Wamethodisti, jinsi ilivyokuwa, nyote mliitwa watakatifu wanaojifingirisha, nafikiri mlijua jambo hilo. Nao wangeingia katika Roho, na kujitupa huku na huko. Nao walisema wao—wao walikuwa na "mishtuko." Wame-. . . Hao, la, hao si Wapentekoste; hao walikuwa Wamethodisti, miaka mingi iliyopita. Nao wakajitupa-tupa, na wakatetemeka, na kuanguka chini ya nguvu za Mungu. Nao wakawatupia maji usoni, na kuwapepea kwa vipepeo, walifikiri wamezimia. Na, sasa, ninyi mlihesabiwa kama kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Bali iliwabidi, baba zenu na mama zenu, aidha iliwabidi kuikubali, kukabiliana na ile Kweli na mambo ya hakika, ama kuikataa.

59 Vipi ninyi Wapentekoste mliopokea kurudishwa kwa vipawa, wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipotokea, pamoja na kunena kwa lugha, na vipawa vya Roho vikirudi kanisani? Mbona, Wamethodisti walitaka kuwafukuza, nao walifanya hivyo. Bali iliwabidi kukabiliana na jambo hilo. Ni jambo lililowabidi kufanya.

Na lile jambo je, lilipotokea, juu ya ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, nanyi mkaona kwamba ilikuwa ni Kweli? Hamna budi kulikabili, ama kufanya jambo fulani juu yake.

Una jukumu, kila mtu analo, nawe huna budi kukabiliana na mambo haya. Vema.

60 Na wakati unapoona basi, katika siku hii sasa, wakati Neno la Mungu limefanya ahadi hizi za mambo ambayo tunaona yakitukia sasa, basi tuna jukumu la aidha kukabiliana Nalo ama kujiepusha Nalo. Huna budi. . .Huwezi kuwa mtu baki. Huna budi kufanya kitu juu ya jambo hilo. Kasema . . .Sharti pawe na kujimudu fulani.

Huwezi kuingia katika mlango huo wa kanisa kisha utoke ukiwa mtu yule yule aliyeingia ndani. Aidha uko mbali sana, ama karibu na Mungu, kila unapoingilia ama kutokea pale.

61 Loo, jinsi ilivyo rahisi kwa watu kuyaepa mambo haya. Nami nataka sisi tuwazie mambo haya tutakapoanza ibada rasmi kesho usiku, kwamba, nawatakeni muone wakati jambo fulani linakabiliwa, kama ninyi . . .kama kuna swali juu ya jambo hilo. Kama kuna swali juu yake, hapana budi kuwe na jibu.

62 Tuseme, kwa mfano, nilisema nilikuwa nikienda magharibi, nawe ukanielekeza upande *huu*. Vema, muda si muda, ninakimbia nipite lengo langu, nami ni ninino sana. . .niko kaskazini-magharibi. Vema, vipi kama mtu fulani akinielekeza upande *huu*, nami niende upande ule? Nitapita lengo langu tena; nilienda kusini-magharibi. Vema, mradi tu kuna swali, magharibi ni upande gani, hakuna budi kuwe na jibu la moja kwa moja mahali fulani.

Na wakati maswali haya yanatukabili, kuhusu Kweli za Biblia, hakuna budi kuwe na jibu sahihi mahali fulani. Hiyo ni kweli. Hakuna budi liwepo.

63 Na wakati tunapoona Jambo fulani limetolewa. Nafikiri, badala ya kukimbia tu, tukisema, "Loo, upuzi, nisingeweza kuamini jambo kama Hilo! Nisingeweza kuamini jambo Hilo." Mbona usichukue Biblia, uketi chini na kulikabili Hilo. Lisome. Uko hapa mkutanoni sasa, lichunguze jambo Hilo tu. Lichunguze, wewe binafsi, kwa Neno. Lichunguze Neno, kwa Neno. Hiyo ndiyo njia pekee ya kulifanya liseme Kweli. Na halina budi kusema Kweli, kutoka Mwanzo hata Ufunuo.

64 Kristo ni ufunuo wa Biblia nzima. Katika Yeye, Kristo, (utimilifu) kutimizwa kwote kwa unabii wa Biblia kunatimilika bila masharti katika Kristo Yesu, kwa maana alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

65 Sasa tunapoona mambo haya, hata hivyo, wakati tunapokabiliwa na tunakuja kwenye mkutano, na tunaona Nguvu za Mungu zikitenda kazi na kufanya mambo, na kufanya kazi za kimbinguni, na kuiona ikifanywa, na kuangalia katika

Biblia na kuona kwamba imeahidiwa kwa ajili ya saa hii; basi tunapoona mambo hayo, ndipo tunakabiliwa na jukumu aidha ya kulikubali, namaanisha, kwa ajili yetu sisi.

66 Sasa, watu wengi wanalionea huruma, watu wengi wanasema ni kweli. Bali jambo hilo—jambo hilo halilifanyi kuwa. . . Hilo silo unalopasiwa. Kama nilivyosema, vipi kama kuna. . .

67 Kama nilikuwa kijana, nami natafuta mke, nipate kumwoa; na hapa palisimama msichana aliye kila sifa niliyodhania kwamba mwanamke anapaswa kuwa nayo. Naam, kiadilifu, alikuwa malkia, na ni mrembo, na—na ana utu wema, ni Mkristo halisi, kila kitu ambacho ningalikiwazia, kujifanyia mke mzuri. Haidhuru ninasema yeye ni mkamilifu jinsi gani, anafaa hasa, yeye si wangu mpaka nitakapomkubali na jukumu la yeye kuwa mke wangu.

68 Hivyo ndivyo Ujumbe ulivyo. Unaweza ukasema, "Ni kweli, ama *hivi, vile,* ama *vinginevyo.*" Kisha useme, "Nalionea huruma. Naamini Hilo ni Kweli." Bali huna budi kuukubali; na huna budi kuwa sehemu yako, nawe uwe sehemu Yake. Huna budi. . . Ndipo, ni wako.

69 Wakati utakapomwoa mwanamke huyu fulani ambaye umemchagua, ninyi ni—ninyi ni mmoja basi.

Na hivyo ndivyo ulivyo na Kristo. Unapomwona amedhihirishwa na kufanywa dhahiri, ndipo wewe u sehemu Yake, Naye ni sehemu yako. Na, pamoja, nyinyi ni sehemu ya Ujumbe.

70 Loo, ni merikebu ngapi za kimadhehebu tulizo nazo zinazoshuka kwenda Tarshishi, kwa ajili ya akina Yona wa siku hizi, mia tisa, na kitu, merikebu zinazochukua njia iliyo rahisi. Hazitaki kukabiliana na jambo hilo.

Yona hakutaka kulikabili, hilo jambo la kwenda kwa Mataifa. Yeye hakutaka kuupeleka huo Ujumbe wa kikatili kule, "Mnamo muda wa siku arobaini, mtaangamizwa msipotubu." Yeye alichukia kufanya jambo hilo. Naye aliwaza, "Hao Mataifa, ni vigumu kusema watakayonifanyia mimi." Bali alipaswa kulikabili. Mnaona? Bali yeye alipanda merikebu rahisi akashuka akaenda Tarshishi, akashuka akaingia pande za ndani za merikebu na akalala; akachukua njia iliyo rahisi.

71 Ni njia rahisi, ni njia inayopendwa na watu. Ni rahisi kuchukua njia ambayo kila mtu atakupigapiga mgongoni na kusema wewe ni jamaa mzuri, "Na huyu ni *fulani wa fulani* na ninino," na ulimwengu utakutazama. Ni rahisi kupitia njia inayopendwa na watu.

Bali inapo—inapokulazimu kufanya jambo ambalo ni tofauti, wakati inapokulazimu kutetea unayoamini kuwa ni

Kweli, hiyo ndiyo sehemu iliyo ngumu, hapo ndipo mkwaruzo unapokuja, papo hapo.

72 Loo, kama vile tumeuimba ule wimbo mzuri mara kwa mara:

> Ni rahisi jinsi gani tunapoabiri bahari, nayo imetulia,
> Kutumainia nguvu za mkono mkuu wa Yehova.

Lakini, loo, hebu mawimbi yaanze kupiga, he—hebu upepo uvume na kuyapiga mawimbi, ndipo unafanya nini?

73 Ni kama kitu nilichoambiwa, wakati mmoja, ambacho bibi fulani alisema. Huko nyuma katika zamani za magari ya farasi, ambaye alisema kwamba farasi alimtorosha, alipokuwa anatoka kanisani. Kasema, "Ulifanya nini?"

74 Kasema, "Nilimtumainia Bwana mpaka kamba zilipokatika." Vema, huo ndio wakati wa kumtumainia Bwana, baada ya kila . . . baada ya kamba kukatika. Unatumainia kamba mpaka zitakapokatika. Naam.

75 Na kwa hiyo tunaona kwamba tuna njia nyingi rahisi za kupitia, merikebu zikienda Tarshishi, kwa maana ni rahisi, kutokujali kitu. Inaingia tu kwa utaratibu, kila kitu ni shwari; kila mtu anakupenda. Na, kila mtu, wewe ni . . . Hakuna anayebishana nawe; wewe hubishani na mtu ye yote. Naam, kama huo si udhaifu na woga mkubwa! Hiyo ni kweli. Naam, sukumia mbali, angusha! Naam, mtu ye yote yule, sijali wewe ni nani, na unachosimamia . . . Kusema kweli, watu wenye mawazo mema watakupenda zaidi kama ukizingatia unayoamini kwamba ni kweli. Sawa. Sijali . . .

76 Unamchukua mwanamke, huenda akawa si mrembo sana, na hata awe nani; bali hebu mwanamke huyo azingatie kanuni za utu uke, hebu asimame kama bibi; na iwapo mwanamume ana wakia wa mwanamume ndani yake, yeye atamtetea mwanamke huyo. Bila shaka. Tunafurahia kitu ambacho—ambacho mtu mwingine anacho, ambacho wanaamini kwamba ni kweli na watazingatia wanachodhania kwamba ni kweli.

77 Uhafifu huo, hivyo ndivyo Wakristo wengi leo, wanashawishika kwa urahisi na kadhalika, hata wanafikiri yote wanayopaswa kufanya ni kujiunga na kanisa, waende mahali fulani, wajiandikishe kwenye kitabu, ama wafanye kitu fulani kidogo, warukeruke, wapige kelele, ama—ama kitu kama hicho, na kuita hicho Ukristo.

Ukristo ni maisha ya kila siku, yaliyo magumu, wakimwishia Mungu katika . . . ulimwengu huu wa sasa. Ni Moto unaowaka daima na upendo wa Mungu, moyoni, ambao unakutia moto na kukuweka kule ng'ambo pamoja na watu, na ukiwavuta watu kwa Kristo. Majukumu.

78 Bali ni rahisi kuipitia njia ambayo ulimwengu unaipitia. Ni rahisi kufuata mkondo.

Unaondoka unaenda kule na kuketi mtoni, na mashua yako. Unachukua makasia yako na kuanza kuyapiga dhidi ya mkondo; huachilii makasia, nayo inakuwa ngumu. Bali achilia makasia mara moja na utaona vile utakavyoipita miti haraka, ukitelemka, bali angalia unakoelekea!

Wakati mambo yanaelea kwa urahisi, kumbuka, unaelekea kwenye—kwenye maporomoko makubwa sana kule chini, ya namna fulani. Unaelekea kwenye maporomoko, na haitachukua muda mrefu nawe utatumbukia kwenye maporomoko hayo. Unaelea tu na ulimwengu, kwa urahisi, jinsi unavyoenda, hutaki jambo hilo. La, bwana. Bali huna budi ku-. . .kukubali jukumu lako.

79 Sasa, unaliamini, nawe una-. . .Unafikiri ni Kweli.

80 Na jukumu ambalo Mungu ametupa katika siku hii, kuuleta ujumbe huu! Na ninapozeeka, na kujua kwamba siku zangu zinakuwa fupi, ninasikia jukumu hilo likiwa kubwa kuliko nilivyowahi kusikia. Tunakaza mwendo, hatuna budi kufanya hivyo! Lazima tuanze kuutekeleza, kila mahala tuendapo, na kuuhubiri Ujumbe; na—na kuwaambia watu ya kwamba Yesu Kristo anakuja, ya kwamba Yeye ni Mungu na yuaja hivi karibuni. Hakuna tu—tumaini lililobakia ulimwenguni ila Kuja kwa Bwana.

81 Nikiangalia nyuma kule kwenye marafiki waliokuwa pamoja nami kule wakati Malaika wa Bwana. . .Hawa wavulana wanaoketi hapa, nafikiri walipapata mahali ambapo jambo hilo lilitukia kule juu. Basi kumbukeni tu jambo ambalo Bwana alisema siku hiyo, akimwambia Ndugu Woods. Wakati alipokuwa akipanda juu ya kile kilima. Na—naye alikuwa kwa namna fulani akilia, kwa kuwa mke wake ni mgonjwa. Ndipo Bwana akasema, "Litwae lile jiwe ukalitupe hewani, na useme, 'BWANA ASEMA HIVI." Nami nikafanya hivyo. Naye Ndugu Woods amekaa kama shahidi.

82 Nami nikasema, "Ndugu Woods, haitachukua muda mrefu kabla hujaona jambo fulani likitukia." Na siku iliyofuata, tulipokuwa tumesimama pale, sisi wote pamoja. . .Na kundi la watu wanaoketi hapa usiku wa leo.

83 Kijana mhubiri alikuweko, naye alikuwa. . .Niliona. . . Ndiyo kwanza nikutane naye usiku uliotangulia. Yeye alikuwa katika kambi yetu. Alikuja apate kuwa pamoja nasi. Naye akaniambia, akasema, "Ndugu Branham, wewe huona maono, huku nje kama mahali hapa?"

84 Nikasema, "Naam, bwana. Bali nimekuja huku kusudi nijiepushe nayo, nipate kupumzika kidogo." Yeye akasema. . . "Vema," nikasema, "Mimi—mimi. . .Bila shaka, Yeye hunionyesha mambo huku nje." Nami nikasema, "Hapa tu juu ya kilima hiki, mahali ambapo wale Malaika saba walipotokea kule chini."

Yeye akasema, "Naam, ninafahamu." Kasema, "Nilikuwa mmoja wa wadhamini wa mkutano wako kule California."

Nikasema, "Vema, bila shaka nafurahi kujua jambo hilo."

85 Na tulipokuwa tumesimama pale, mara nikaangalia na kuona namna fulani ya daktari mnene akiyachunguza macho yake, ndipo nikamsikia akisema, "Utapoteza jicho hilo, kwa maana mle ndani mna wepesi wa kuambukizwa. Nami nimelitibu kwa muda wa miaka miwili, nawe utapoteza jicho hilo."

Nikasema, "Sababu ya kuniuliza jambo hilo, ni kwa sababu daktari wako alikwambia hivi majuzi utapoteza jicho hilo."

Naye akasema, "Hiyo ni kweli," naye akatazama kila mahali namna *hiyo*.

86 Nami nikamwona mama yake akitoa moja ya soksi zake ndefu na kuunyosha mguu wake, huku vivimbe vidogo vikining'inia katikati ya vidole vyake vya mguu, huku na huko kwenye mguu wake; kisha akasema, "Kama ukimwona Ndugu Branham, mwambia aliombee hili."

Nami nikasema, "Mama yako alinyosha ninino wake... aliunyosha mguu wake namna *hiyo*, na kusema alikuwa na... ana vivimbe vidogo kila mahali kwenye vidole vya—vyake vya mguu, na namna hiyo; ndipo akasema, 'Mwambie Ndugu Branham aniombee.'"

Akasema, "Ndugu Branham, hiyo ni kweli."

87 Nikaangalia nyuma. Nilipoangalia, nikamwona amesimama pale ananiangalia, namna *hiyo*, macho yake yakiwa maangavu kabisa. Nilikutana naye kwenye majira haya ya kupukutika majani; alikuwa na macho mazuri zaidi kuliko mtu ye yote kambini. Bwana alikuwa amemponya na kumpa afya.

88 Nilipokuwa nimesimama pale, Bwana akasema, akanionyesha yatakayotukia. "Hukumu iko tayari kuipiga Pwani ya Magharibi." Naye akasema, "Ondoka uende kule, karibu na mekoni."

89 Nami nilikuwa na sepetu mkononi; nikaondoka nikaenda pale. Naye Ndugu Roy Roberson, sisi sote tunamjua hapa. Hayuko hapa usiku wa leo, nijuavyo mimi; yuko huko Arizona. Yeye ni mwenyekiti wa wadhamini hapa, nami nilimjua kwamba ni shujaa wa vita. Na jambo fulani lilikuwa litukie; asubuhi nzuri sana, na tulivu yapata saa nne asubuhi. Nao hao wavulana wamepazunguka mahali pale, tukiwa kumi ama kumi na wawili, tuking'oa mahema, na kuchuna nguruwe, na kadhalika. Kwa hiyo sisi...Nikaenda hapa na pale, nikasema, "Roy, jifiche, haraka. Kitu fulani kiko karibu kutukia." Nisingeweza kumwambia zaidi. Bali wakati tu nilipofika pale...

Kisha upepo wa kisulisuli wa Mungu ukashuka ukaja kutoka mbinguni, ukanguruma, kama ngurumo, ukavitikisa vilima,

ukaenda kasi kwenye mlima huo, ukakata mstari moja kwa moja kuuzunguka, yapata futi tano juu ya kichwa changu, na ukakata vilele vya miti hiyo, huku mawe yakirushwa nje. Ukapaa juu hewani kisha ukashuka ukaja tena, ukiwa na ubatizo mwingine mkubwa, ukapiga milimani, na kuyarusha mawe nje namna hiyo. Ulifanya hivyo mara tatu, kisha ukapaa juu hewani.

Ndipo Ndugu Banks akanijia mimi, kasema, "Hivyo ndivyo ulivyosema jana?"

Nikasema, "Naam, bwana, hivyo ndivyo hasa." Mnaona?

90 Ndipo siku mbili baada ya hilo, Alaska ikazama, karibu izame, kule juu. Na huku na huko kwenye Pwani ya Magharibi kumekuwa na ngurumo na misukumo, na kila kitu kikitukia. Na hivi karibuni itazama chini ya bahari. Hiyo ni kweli. Ni nini? Tunaishi katika saa ya Kuja kwa Bwana.

91 Tunapoona itikadi na mengineyo yakitukia, na mambo haya yote mbalimbali, tunajua hapana budi kuwe na jibu halisi juu ya jambo hili.

Kuna watu nje huko nchini sasa, wanaingia mapangoni na kadhalika, "Na tarehe 16 Marchi," mumesoma kisa hicho katika magazeti, "Bwana yuaja." Mnajua jambo hilo sivyo lilivyo.

Yesu alisema, "Hakuna mtu aijuaye ile dakika wala hiyo saa."

92 Tunapoona mambo haya yote, na mambo yakitendeka jinsi yanavyotendeka, na hapana budi pawe na jibu la kweli mahali fulani. Hapana budi pawe na Kweli. Kuna moja, mashariki; na nyingine, magharibi; bali kuna moja, kusini-mashariki, na kasikazini-magharibi, ama kitu fulani. Bali hapana budi kuwe na jibu la kweli, mahali fulani, kwa hilo swali. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

93 Tujiepushe na jambo hili? Lazima tuwaambie watu ya kwamba tunaishi katika saa za Kuja kwa Mwana wa Mungu. Tunataka—tunataka kukesha na (Mungu) tuwe tunasonga mbele, kila wakati, tukiwa tayari kumpa mtu jibu sahihi.

94 Daima imekuwa namna hiyo. Ime—imekuwa katika mwanadamu, amejiepusha na akaenda mbali na Mungu, tangu wakati wa Adamu, katika bustani ya Edeni. Wakati Adamu alipokuwa katika bustani ya Edeni, wakati alipofikia jukumu la kufanya chaguo lake, je, yeye angekaa pamoja na Mungu ama ataandamana na mkewe? Ilimbidi kufanya hilo juku-. . . ilimbidi kufanya hilo, ju—jukumu lilikuwa juu yake. Aidha ilimbidi kuchukua alichosema mkewe ama alichosema Mungu. Na alipochagua kuifuata njia ya mkewe, basi alipofanya hivyo, ndipo alipoteza hali yake ya asili. Kisha akauleta ulimwengu mzima chini ya mauti, wakati alipopaswa kuchukua jukumu, ama achukue nuru mpya ambayo mkewe alikuwa ameipata, ambayo ilikuwa ni kinyume.

Ee Mungu! Wazia jambo hilo. Mungu aliwapa tu kama Maneno manane ama kumi kutii. "Bali ya mti huo hamtayala." Hayo ndiyo tu waliyopaswa kutii. Na hata pamoja na . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . Neno zaidi, wao walilitangua.

Ndipo ilimlazimu Adamu kukabiliana na, "Mimi, mimi nitafanya kama mke wangu alivyosema nifanye, ama nitafanya aliyosema Mungu nifanye?" Naye akaondoka akaenda huku ameyafungua macho yake. Ilimbidi kuchukua jukumu. Jambo hilo likaitupilia jamii yote ya binadamu katika mauti.

95 Ndipo akaja yule Adamu mwingine, ambaye ni Kristo, hapajatokea Mmoja kama yeye! Mtu fulani anasema Yeye hakuwa Mungu? Kutokuwa Kwake na kifani kulithibitisha ya kwamba alikuwa Mungu. Hapajatokea kiumbe kilichoishi kama Yeye. Yeye aliishi katika ulimwengu Wake Mwenyewe. Yeye alizaliwa nje ya ulimwengu wa kawaida . . . ? . . . Haleluya! Yeye Mwenyewe ni Muumba aliyefanyika mwili.

Ni nani angaliweza kusimama mahali Yeye aliposimama? Ni nani aliyewahi kuzungumza kama Yeye. Ni nani angeweza kusema mambo aliyosema? Ni nani angaliweza kutenda mambo aliyotenda? Kutokuwa Kwake na kifani kulithibitisha kwamba alikuwa Mungu. Hapakuwepo na nabii ama cho chote kile ambacho kingeweza kufanya aliyofanya Yeye; ni Nani angaliweza kuwaita wafu kutoka kaburini, na ni Nani angeweza kuzifunga mbingu, na kufanya lo lote alilotaka kufanya. Yeye alikuwa Mungu. Ni nani angaliweza kusimama mahali Pake? Nani? Yeye angekuwa nani ila yule Mungu mkamilifu na asiyepatikana na mauti, aliyefanyika mwili na kukaa kati yetu!

96 Hakuna kitu kiliweza kulinganishwa Naye. Yeye aliishi katika ulimwengu Wake Mwenyewe. Hakuna mtu aliyewahi kunena kama Yeye. Alipokifungua kinywa Chake tu, kuna kitu juu yake, ambacho kilikuwa tofauti na mtu mwingine ye yote. Mtu fulani alisema alikuwa tu mtu wa kawaida; nakanusha jambo hilo. Yeye alikuwa Mungu. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Kwa maana, hakuna mtu aliyewahi kunena kama Yeye, hakuna mtu angaliweza kunena kama Yeye, kwa maana alikuwa Neno lililo hai Lenyewe lililofanyika mwili, udhihirisho wa utimilifu wote wa Mungu.

97 Nitakubali, hao manabii walikuwa na ujumbe wao. Walikuwa nazo wakati huo; wanazo sasa. Bali kulikuweko na utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili, umedhihirishwa pale. Yeye alikuwa asiye na kifani, Naye ndiye ambaye alipaswa kukabiliana na jukumu hilo. Akiwa na nguvu Zake zote kuu alizokuwa nazo, hata angaliweza kuwa mfalme wa ulimwengu kabisa. Yeye atakuwa hivyo; Naye, kwa watakatifu Wake, ndivyo alivyo sasa.

98 Yeye alisimama pale. Ni mtu gani angalikua maskini, hana mahali pa kulaza kichwa Chake; ambaye hata alijua

mahali samaki alikuwa amemeza sarafu. Ni nani, ni mtu gani angaliweza kuichukua hiyo mitungi mikubwa ya maji na kuigeuza ikawa divai, na asiwe na mahali pa kulaza kichwa Chake? Ilimbidi kukabiliana na majukumu yaliyokuwa yamewekwa mkononi Mwake. Ni mtu gani angaliweza kumfufua mtu kutoka kaburini, baada ya kufa kwa muda wa siku nne na ameoza?

Je, Yeye hangeweza kujiokoa Mwenyewe? Bila shaka, angeweza; lakini kama angefanya hivyo, asingalituokoa. Ilimbidi kuyakabili majukumu, na kwa sababu ya kutii Kwake Neno! Ambapo, kutokutii kwa Adamu, naye alikuwa amechukua njia ya mkato, nji—njia ya kushuka kwenda Tarshishi. Bali Yesu alichukua njia ya kwenda Ninawi, kwa Mataifa, kujipatia Bibi-arusi. Nina furaha kwamba Yeye alifanya hivyo, usiku wa leo. Nasi inatubidi kuyakabili mambo ya hakika, ya kwamba sisi ni mali Yake, na tuuondoe ulimwengu. Amina!

99 Kila mtu ilimbidi kukabili jambo hilo, ambaye ana jukumu mbele ya Mungu. Tuchukue tu, kwa mfano, Nuhu. Yeye alilikabili. Nuhu, Musa, Eliya, na hao wengine wote, kila wakati, iliwabidi kulikabili jukumu. Nao walipaswa kufanya jambo hilo, lakini hiyo ndiyo sababu walitumwa kwenye ile saa.

100 Mtazame Nuhu katika kizazi chake cha kisayansi, jinsi ilivyombidi kulikabili jambo lililokuwa si la kisayansi kabisa. Mbona, hapakuwepo na sa—sa—sababu ya ni kwa nini halingekuwa lisilo la kisayansi. . . Mnaona, li—lilikuwa lisilo la kisayansi, hasa. Mbona, wao walisema itanyesha kutoka angani. Wao hawakuwa wamepata mvua iliyonyesha kutoka mbinguni. Sasa, ilimbidi kukabiliana na jambo hilo. Mungu alisema itanyesha. Kisha yeye aka-. . .

101 Ndipo imani bila ya matendo imekufa; kama ukisema, "Ninaliamini," na hutendi tendo lo lote. Ni kama tu Ujumbe, kama ukisema, "Ninauamini," hufanyi tendo, una faida gani? Mnaona? Nuhu alienda kufanya kazi na nyundo yake na akajenga safina, kuthibitisha alilokuwa anazungumzia. Hilo ndilo litupasalo kufanya, pia. Hatuna budi kufanya kazi na kuthibitisha imani yetu, kwa matendo yetu. Matendo yetu yanathibitisha imani yetu.

102 Ilimbidi Musa kufanya hivyo, na ilimbidi Eliya kufanya hivyo. Kila nabii katika wakati wake ilimbidi kusimama na kukabiliana na majukumu haya. Bali wengi wao hawakufanya kama Yona. Yeye alitoroka; wao hawakutoroka.

103 Tazama, "Ukapige kelele juu yake." Loo, jamani! Hilo hapo. Hilo ndilo somo, "Ukapige kelele juu yake." Hiyo hapo sehemu ya kuthibitisha haki.

Nenda tu kule ukawaambie jamaa hao, "Aisee, nimeshuka kuja kujiunga nanyi enyi jamaa. Mnajua, naamini nitawaambia nitakachofanya. Nina kitu kidogo tu hapa naamini ninaweza

kuifanya ninino . . . kutuunganisha sote pamoja, na kufanya *hivi, vile,* ama *vinginevyo*."

Bali, ilikuwa, "Ukapige kelele juu yake," inapokubidi kupiga kelele juu ya jambo fulani. Sasa, ilimbidi kupiga kelele juu ya kila kitu kilichokuwa kule; kupiga kelele juu ya ule mji, kupiga kelele juu ya matendo yao, kupiga kelele juu ya kanisa lao, kupiga kelele juu ya manabii wao, kupiga kelele juu ya wahudumu wao, kupiga kelele juu ya makasisi wao. "Ukapige kelele juu yake, kito hicho chote! Ukapige kelele juu yake!"

104 Nuhu alipiga kelele juu ya wakati wake. Bila shaka, alifanya hivyo, juu ya makanisa ya wakati wake.

Musa bila shaka kabisa alipiga kelele juu ya wakati wa—wake; hao watu, makuhani, na kadhalika. Yeye alipiga kelele kote kote jangwani. Na kila njia panda, yeye alipiga kelele, daima akipiga kelele kwa hao watu.

Eliya alichukiwa sana katika kizazi chake, kwa maana yeye alipiga kelele juu ya kizazi hicho. Bila shaka alipaza.

105 Yohana Mbatizaji alichukiwa sana katika kizazi chake. Yeye alipiga kelele juu ya wakati wake. Yeye alimwambia mfalme, m—mtawala wa—wa ile nchi; yeye—yeye alikuwa, alimuoa mke wa ndugu yake. Ilimbidi kuhubiri juu ya ndoa na talaka, asubuhi moja. Kwa hiyo alipiga kelele juu yake, akasema, "Si halali wewe kumchukua." Ilimgharimu, kichwa chake kukatwa, baadaye, bali yeye alipiga kelele na akasimama kwenye wajibu wake.

Yeye hakuchukua merikebu ya kwenda Tarshishi, na kusema, "Vema, nitakubaliana nawe, Herode. Ni sawa. Mradi tu unafikiri yeye ni mwanamke mzuri, anakuwa mke mzuri kwa ajili yako, endelea." Loo, rehema. Hao watu hafifu na waoga, mnaona, naam, kila kitu kilicho kidogo tu . . . Kitu kidogo, mbona, hakina faida ila ni cha kusafisha sahani zilizo chafu.

106 Bali, angalia, Yohana hakuwa namna hiyo. Yeye alikabiliana nalo. Yeye alisema, "Si halali kwako kumchukua." Naam, bwana. Naye akalipinga jambo hilo.

107 Wao hawakukimbia kamwe. Yohana hakufanya hivyo. Wao walisimama na kukabiliana na ukweli wa mambo. Musa alijaribu kukimbia, wakati mmoja, kama Yona, bali Mungu alimrudisha. Wengi wao walijaribu kuepukana nalo; wao wangeanza . . .

Lakini, angalia, kama Mungu amekuita, nawe una hakika ya kwamba Mungu yuko katika Ujumbe, hakuna kitu kitakachokurudisha nyuma. Haikumrudisha Yona nyuma. La, bwana.

108 Amosi wa kale, alipiga kelele, kasema, "Simba amekwisha kunguruma, ni nani asiyeogopa? Pia Mungu amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?" Ni nani awezaye neno ila kutabiri,

unapoona Mungu akinena na akasema jambo fulani litatukia, na hilo hapo?

109 Simba anapolia, kila mtu anaogopa, naam, bwana, iwapo umeshasikia mlio mmoja msituni. Unaweza kusikia hii milio ya paka kwenye matundu haya huku nje, hao simba wa kufugwa, bali wapaswa kusikia mngurumo mmoja ulio halisi na wa mwitu wakati mmoja. Miamba itaanguka kutoka kilimani, umbali wa yadi mia tano. Sioni sehemu huko kupiga mbweu kwote kunakotoka kwenye hayo mapafu. Naye hukitupa kichwa chake chini, anatupa hayo manyoya juu; sijasikia kitu . . . Kama m—mzinga ukilia, wakati anapopiga mbweu na huo mlio mkubwa katika mapafu yake. Ni nani asingeweza kuogopa?

Wao wanasema, kama ukipata kuuawa na simba, huoni maumivu. Anakuogofya hata kufa kabla hajakufikia. Mnaoana, wewe hujisikii. Yeye hukuogofya kwa huo mngurumo mkubwa na mkali, naye huyu hapa amekuvamia katika nukta moja.

110 Yeye alisema, "Simba amekwisha kunguruma, ni nani asiyeogopa? Naye Mungu amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?" Unapomwona Mungu akifanya jambo fulani, unasema . . . "Huenda nisiwe nabii . . . " Yona alisema . . . "Huenda nisiwe nabii, ama mwana wa nabii. Bali Mungu amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?"

111 Huenda nisiwe nabii, huenda nisiwe *hiki, kile,* ama kile *kingine*. Ninapomwona Mungu akifanya cho chote, na ninakiona hapa katika Neno, Naye alikiahidi, ni nani wawezao kunyamaza na kutulia? Bila shaka, Yeye amefanya hivyo.

112 Wala sisi nasi hatuwezi kujificha nyuma ya kanuni za imani na mashirika haya yote hapa, na kushuka kwenda—kwenda Tarshishi. Hatutaki kuambatana na hayo mashirika.

113 Bali wengi, kama Adamu, wanafanya jambo lile lile, wanajaribu kufanya badilisho kwa njia fulani, wanajaribu kupata njia ya kuepukia, na—na kufanya badiliko, kukabiliana na Mungu. Baada ya wao kujua, wakiwa makosani, wakikabiliwa na Kweli, akaambatana na mke wake na kufanya yale hasa Mungu aliyomwambia asifanye. Yeye aliondoka akaenda na kuyafanya, hata hivyo. Ndipo akajikuta yu uchi, yeye na huyo mwanamume, wote wawili, katika bustani ya Edeni. Macho yao yakafunguliwa. Wakajua mema na mabaya, wakati huo. Ndipo akajaribu kupata kibadilisho, kusudi ajifunike mwenyewe kwa njia fulani kwake.

Sasa, hivyo ni kama vile tu tunavyofanya leo, huo udhuru, kusema, "Vema, nakwambia, kama ilikuwa *hapa*, ama kama *hii*." Ama, "kama, kama, kama," hiyo ni tu . . . Mnaona? Bali huna budi kukabiliana nalo. Aidha ni kweli ama ni uongo. Na kama ni kweli, hebu tudumu nalo. Iwapo ni uongo, liondokee. Hivyo tu. Pata ambalo . . . Chunguza lililo kweli. Hutaki kungojea zaidi.

Hebu na tuone sasa ukweli ni upi na lililo sahihi, na tudumu nalo. Tunajua ni kweli.

114 Sasa, tunaona ya kwamba leo watu wetu ni ninino sana . . . Inaonekana kama kwamba unyofu wote wa moyo umetoka makanisani. Mimi . . . Katika . . .

115 Tunaishi katika nyumba pale ya dada wa thamani anayehudhuria kanisa hili. Labda ameketi hapa usiku wa leo. Naye anaikodisha kwa ninino yake . . . watu. Naye amekuwa tu mwema sana kwetu kuhusu mahali pale, kuhusu kutuacha tupachukue mahali pale. Na kwa hiyo ningetaja jina lake, lakini huenda asitake mimi nifanye hivyo. Naye amekuwa mwema sana kwetu, vema, bila shaka sisi hatunge—hatungetaka kumtangaza. Bali amekuwa mwanamke mpendwa sana, sana. Na kule nyumbani, kulikuweko na televisheni upande mmoja. Tuna nyumba ndogo yenye, viwili, yenye vyumba viwili.

Nina jamaa kubwa, na kundi la watoto wadogo, nasi . . . na mwa—mwajua, hawana budi kuwa na vitanda, na vingi sana. Na kila kitu kimerundikwa juu yake, na huna budi kutembea kupitia *hiki* na kupitia *kile*, kuingia na kutoka.

116 Halafu kule walikuwa na televisheni. Na katika televisheni hii, watoto hawa wakaanza kuitazama, Jumapili asubuhi, kikaja kipindi cha namna fulani cha kuimba nyimbo za dini. Ndipo, mwajua, nu—karibu ikufanye uone aibu; kama hakungalikuwa na Ukristo halisi mahali fulani ambao ungeweza kushikilia, kuona kile kinachoitwa Ukristo. Mbona, inaonekana kana kwamba unyofu wote wa moyo umekwisha mle. Mbona, hao, hao hawaonekani kama . . . Mbona, ni jambo baya sana tu jinsi wanavyosimama pale na kukunja ngumi zao na kupigana wao kwa wao, pale, na kujaribu kuimba nyimbo za dini na kila kitu namna hiyo; na kufanya utani ambao ni vigumu kwa baharia kufanya, na kusema mambo ya kila namna, na kucheza na kuendelea. Mwajua, utakatifu wa—wa—wa Ukristo unaonekana umepoteza mahali pake.

117 Sasa, mimi huenda kanisani na—na kuona mchungaji akiondoka anaenda pale na kutangaza ya kwamba ku—kutakuwa na mashindano ya ku—kuogelea. Wanawake wote katika hizi nguo za kuogelea, wote wanaondoka wanaenda kule. Watakuwa na mashindano; hawa wanawake, kuogelea. Nao watakuwa na ka—karamu ya namna fulani, nao watakaanga ku—kuku wengi sana, na kucheza karata, na—na mambo haya yote namna hiyo. Kwangu mimi, jambo hilo linaondoa unyofu halisi kutoka katika Ukristo; kuruhusu tu kila kitu.

118 Nimeona, tukija hapa, tunaona . . . Mwajua, tunaona wengi zaidi wa dada zetu wakivaa kaptura, huku katika nchi hii ya baridi, kuliko unavyowapata nje huko katika nchi ile yenye joto. Mnaona, ni kweli. Huko nje ambako ni joto kweli, hakuna wengi sana wa hao wanaozivalia. Bali hapa,

ambapo—ambapo ni baridi, wao—wao wanafanya hivyo. Mnaona, ni, wao hawatambui ni ibilisi anayefanya jambo hilo. Mnaona? Sasa, kama ilikuwa ni kustarehe, kama ilikuwa ni kwamba unajisaidia, ingekuwa ni jambo lingine. Ikiwa ni mwnamume, nafikiri inaonekana ni kitu cha kuchefusha moyo mwanamume akiivalia, lakini—lakini wewe—unge-— usingelimjali mwanamume. Lakini, bibi, mwili wa—wake ni mtakatifu, na hana budi kuuweka namna hiyo. Na kuona mzee . . .

119 Mnaweza kuona, watu leo. Kuna roho wawili. Na moja ni Roho Mtakatifu; na huyo mwingine ni pepo mchafu, na mmoja anatawaliwa na huyo. Na wote wawili wa kidini. Sasa, naam, hiyo ndiyo sehemu ya kushangaza, wote wawili ni wa kidini. Na kama tu vile Esau na Yakobo walivyokuwa, wote ni wa kidini, kama vile Kaini na Habili walivyokuwa, wote wawili ni wa kidini; kama walivyokuwa Yuda na Yesu, wote wawili ni wa kidini, wote wawili ni wa kidini. Na tunaona hilo leo, pande zote mbili, za kidini. Mnaona, ni roho yule yule. Hao watu hufa, bali huyo roho hafi. Anaendelea moja kwa moja, wote wawili ni wa kidini.

Mmoja amejazwa na Roho Mtakatifu, ambaye anaishi maisha wanayopaswa kuishi, na kuenenda kitauwa na kwa uaminifu. Hawawezi kukunyang'anya hata hela, nao—nao wanafanya kila kitu kwa uminifu wawezavyo, kukusaidia. Na hao wengine wata- . . . Ni wema tu wawezavyo kuwa.

Na hao wengine, tunaona, ni vinginevyo tu. Na, hata hivyo, wote wawili ni roho za kidini, hao wawili, mmoja, Roho Mtakatifu; na huyo mwingine, roho mchafu. Na kama uliangalia, itakuwa, hata ingawa wanajidai ni wa kidini, watakufanyia mzaha na kukuita mtakatifu anayejifingirisha. Wanafanya cho chote wawezacho.

120 Wao, wakipuuza Ne—neno la Mungu lisilobadilika, kama kwamba halijaandikwa kamwe.

Mnaona, mnaweza mkasema, "Sasa, angalia hapaMtakatifu!" ubatizo . . . "

"Nina Roho Mtakatifu!"

"Na huku unasimama pale na msokoto huo mkononi mwako, ukiuvuta?"

"Ndiyo, nina Roho Mtakatifu! Sidhani ni kosa kunywa pombe kidogo. Sidhani ni . . . " Mnaona?

Na hivi mliona, "Sidhani"? Bali Mungu anadhania vingine, mnaona, kulingana na Neno Lake. Mnaona? Mnaona, wao . . . Nao—nao ni kama tu kwa urahisi wana—wanalitemea mate. Hiyo ni kweli hasa.

121 Ni kama tu vile huyu maskini jamaa kilema wa kale alivyojikokota akatoka wakati ule, wakati Daudi alipokuwa

anafukuzwa kutoka kwenye kiti chake cha enzi. Yeye alikuwa anakwea Mlima wa Mizeituni, akiondoka, huku analia akiukwea, akiangalia nyuma. Na maskini jamaa huyu mzee akajikokota akatoka pale naye alikuwa anamtemea mate. Ndipo yule mlinzi akasema, "Nitakiacha . . . kichwa cha mbwa yule kikae juu yake, huku amemtemea mate mfalme wangu?"

Daudi akasema, "Mwache." Mnaona, walimtemea mate.

122 Yapata miaka mia nane baadaye, wao wakamtemea mate mwanawe, Yesu Kristo, pia.

Na leo wao wanalitemea mate tena, kama tu kwamba hata halikuwa . . . Hawana kicho, hawajali, wanageuza tu vichwa vyao na kuondoka Kwake, na kucheka mbele zako. Ni kwa nini? Wao wako kwenye merikebu inayoelekea Tarshishi. Hiyo ni kweli.

Mwito huu wa Mungu, huna budi kupiga kelele juu ya maovu, kupiga kelele juu ya dhambi, kupiga kelele juu ya mambo yaliyo mabaya. Naam, kumbuka, itakuwa hivyo.

Jamani, mnajua, wakati huu. Mnajua, nina tofauti ya masaa mawili. Na huko Tucson ni saa moja tu na dakika kumi, na—nami kwa namna fulani ninakuwa—kwa namna fulani siko mahali pangu hapa sasa. Vema.

123 Sasa kumbukeni, itatubidi kuwajibika kwa jambo hilo. Kumbukeni, wale wanaomtemea Kristo mate huwajibika.

Wakati Daudi aliporudi kutoka kwenye uhamisho wake, alipokuwa mtoro, na aliporudi, kumbukeni, jamaa huyu alianguka kufudifudi na kuomba rehema. Yeye alimtemea mate Daudi, alipokuwa anaondoka, bali alikuwa karibu tayari kuiosha miguu yake kwa majonzi, na wakati aliporudi.

Na siku moja wale ambao wamemchoma Yesu watajuta.

Na wale wanaomchoma leo watajuta, pia. Wao, siku moja, itarudi. Kumbukeni, Ufunuo 22, Yeye anatutaka kutii kila Neno ambalo limeandikwa; kila Neno.

124 Sasa tunajua Uwepo Wake uko hapa. Umethibitishwa. Sisi tunao. Tunatumaini, katika juma hili lijalo, utaendelea kuthibitishwa miongoni mwetu; wagonjwa wataponywa, na mambo makuu yatakuwa yakitendeka.

Hatutaki wazo linalopendwa na watu wengi. Tunataka Ukweli. Nasi hatuninino, tuna(taka) hatutaki ku-—hatutaki kukabili cho chote ila ambacho Mungu amesema ni Kweli. Lakini, "Ujue ya kwamba dhambi zako daima zitakudhihirisha." Kama hazikudhihirishi hapa, zitakudhihirisha kwenye ile Hukumu. Kwa hiyo wewe—wewe . . . Zitakupata mahali fulani, sasa. Naam, bwana.

125 Bali kama wewe ni Mkristo halisi, aliyeitwa kweli kama Yona alivyoitwa, Mungu tayari amekulipia nauli yako. Toka

kwenye merikebu hiyo inayoelekea Tarshishi, hata hivyo. Mungu alikuchagua tangu zamani kwa ajili ya maisha haya. Naam, bwana. Kama wewe ni mwana wa Mungu ambaye ni wa kweli na aliyeitwa, njoo Kwake Kristo. Njoo kwenye utimilifu Wake. Safari yako imelipwa mpaka wapi? Imelipwa mpaka Ninawi, si kwenda Tarshishi. Wewe umechaguliwa tangu awali. Merikebu yako. . .Kuna merikebu inayoondoka sasa hivi, iko njiani. Kwa hiyo kuna jambo moja tu la kufanya, ni kuingia ndani yake. Na kama ulikuwa kama Mungu, hutapata amani kamwe. . .

126 Kama maskini mpwangu, muda kidogo uliopita. Kama miaka kumi sasa, amezurura sana. Asubuhi moja anaenda kwenye kanisa hili, kanisa hili la Katoliki chini hapa, na kuchukua hili kwa sababu ya vile baba mtakatifu fulani anayenena habari zake hapa, na wengine *hapa*, na wengine *hapa*. Jumla ya hayo yote ni nini? Mnaona? Na sasa angali anaona njaa na kuona kiu. Nikasema, "Mahali pako ni hapa kwenye madhabahu, mwanangu." Mnaona?

Hakuna njia ya kutoka katika jambo hilo. Wakati Mungu anakufuatilia, afadhali hata ujitoe na kuendelea. Hivyo tu.

127 Kumbukeni, Mungu! Vema, Mungu alikuwa kwenye ile merikebu. Mungu alikuwa kwenye ile tufani. Mungu alikuwa katika yule samaki. Kila mahali alipogeuka, Mungu alikuwepo.

Mnaona, Mungu yuko, na itaendelea tu kukusumbua. Kwa hiyo kwa nini tunangojea zaidi? Hebu na tuanze ufufuo huu vizuri. Hiyo ni kweli. Mnangojea nini? Tunaamini ya kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia, Naye atakuwa na Bibi-Arusi, na Yuko tayari. Nasi hatutaki merikebu zo zote zinazoelekea Tarshishi ye yote. Tunaenda Ninawi. Tunaenda Utukufuni. Amina. Hiyo ni kweli. Tunaelekea mahali ambapo Mungu atatubariki, na hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya.

128 Tukae katika Uwepo wa Mungu, basi, kwa mioyo yetu; si mikono yetu, sana, bali mioyo yetu mbele ya Mungu, mpaka ametukoleza, kabisa kabisa, namna hiyo, na hiyo nuru ya utukufu Wake; na kutuoka tukawa ninino Yake—wema Wake, na akakiivisha kile tulicho nacho, kikawa halisi, mnaona, kufikia mahali ambapo tunaweza kuwaonyesha wengine ya kwamba Yesu Kristo yu hai. Loo, jamani! Tunataka kuamini jambo hilo.

129 Pia kumbuka, mahali Yona alipokwenda, Mungu alikuwa katika ile merikebu; Mungu alikuwa katika ile tufani; Mungu alikuwa katika yule samaki. Aliendelea kuwa pamoja na Yona hata mapenzi Yake makamilifu yakafanyika. Hiyo ni kweli.

Na kama Yeye atakufuata kamwe, unaweza ukaepa *hapa*, na kuepa *pale*, bali utakuwa mwenye mashaka mpaka utakaporudi na kufanya jambo ambalo ulianza kwa ajili Yake kwanza. Mnaona? Usiende, usijiepushe na Uwepo wa Mungu. Ukabili. Unaamini ni Kweli, basi hebu. . .Kama ni Kweli, linastahili kuishiwa, kufiwa, cho chote kile. Na kama Yeye amelithibitisha

kwako kamwe, ya kwamba ni Kweli, basi hatuwezi kujiepusha nalo, po pote. Yeye atakuwa pale pale, vile vile. Huwezi kufanya hivyo.

130 Kwa nabii Wake aliyemtoa, yule aliyemtuma kushuka kwenda kule na kuutangaza ujumbe huo. Naam, ilionekana kama kwamba Yeye angaliweza kumtuma nabii mwingine, bali Yeye alimchagua Yona; na hata Eliya asingalifaa; Yeremia asingalifaa; Musa asingalifaa. Yona ndiye ilikuwa aende Ninawi. Hakukuwa na lingine. Yeye alimwagiza na kumwambia aondoke aende. Na Yeye anaposema, "Nenda kule, Yona, nenda Ninawi," hakuna mwingine anayeweza kwenda kufanya jambo hilo ila Yona.

Na wakati Mungu anapokwambia jambo fulani, huna budi kulifanya; hakuna mwingine. Mnaona, hatuna budi kukabiliana nalo, na, kisha twende tukalitende.

131 Tunaamini ya kwamba tunaishi katika saa ambayo Mungu anafanya jambo fulani. Tunaamini ya kwamba tunaishi miongoni mwao sasa. Ninaamini usiku wa leo ninahubiria kusanyiko lile ambalo—ambalo linakaa, linangojea kule lipate tu kuiva. Kwe—kweli ninaamini jambo hilo, kwa moyo wangu wote. Ningesema liko sasa jinsi ile ile limekuwa daima.

132 Sasa, tunaamini ya kwamba saa imewadia ambapo Yohana Mtakatifu 14:12 haina budi kutimizwa. Sisi, tunaamini ya kwamba Malaki 4 haina budi kutimizwa. Tunaamini ya kwamba Luka 17:30 haina budi kutimizwa. Tunaamini jambo hilo, nabii hizi zote ambazo Yeye alisema zingetimia katika wakati huu. Tunaamini hazina budi kutimizwa, na tunaamini tunaziona zikitimizwa sasa hivi. Hiyo ni kweli kabisa.

133 Acha kukimbia. Usitoke katika Uwepo Wake; ingia tu katika Uwepo Wake. Hiyo ni kweli. Nami najua hivyo ndivyo unavyotaka kufanya. Maana, nimeona leseni kule nje kutoka Texas, kutoka Louisiana, na kila mahali. Hilo ndilo lililotuleta hapa, si kujiepusha na Uwepo Wake, bali kukimbia na kuingia katika Uwepo Wake.

Rudi, toka kwenye. . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . umekuwa Yona, kama umekuwa ukishangaa upitie njia gani ama ufanye nini, fanya hima, ingia kwenye merikebu pamoja nasi usiku wa leo. Tunashuka kwenda Tarshishi, kupiga kelele . . . ama, Ninawi, kupiga kelele. Tunaiacha hiyo merikebu ya Tarshishi ishuke iende kama wakitaka. Tuna wajibu mbele za Mungu, huo ni, Ujumbe ambao tunawajibika kwake.

134 Kwa hiyo juma hili lijalo, ni utangulizi mdogo tu usiku huu, kwa kuwajulisha. Ninapopiga kelele, ninawajibika peke yangu kwa Ujumbe fulani, ndugu. Ninyi wahudumu mnaoketi hapa, siko hapa kuwaudhi. Nanyi wanawake na wanaume, juu ya kisa hiki cha ndoa na talaka kinachokuja, nawatakeni mkumbuke

usiku wa leo. Nimesema mambo haya yote, kuwaeleza jambo hili, ya kwamba mimi ninawajibika tu kwa Mungu.

Na halafu, tena, mimi ninawajibika kwenu, kuwaambieni Kweli. Nami sitawaambia kitu ila kweli, mradi tu Mungu ananiwezesha kujua Kweli ni nini. Mpaka nitakapojua Ukweli, sitasema neno juu yake, mnaona, sitasema kitu juu yake. Bali ninaamini ya kwamba Mungu ananionyesha Ukweli juu ya *Ndoa na Talaka*, nami ninatumaini ya kwamba Yeye ataniruhusu kuuleta.

135 Na Jumbe zingine ambazo ninatazamia kuwa nazo juma hili, ni *Huyu Melkizedeki Ni Nani? Mungu Alichagua Mahali Gani Kuweka Jina Lake?* Na vichache vya vitu hivyo namna hiyo, ambavyo ni Jumbe zinazokuja, na *Utungu wa Kuzaa*. Na—na mambo machache, ambayo ni ya—ya namna hiyo, na ambayo yanaongezea kwenye *Mwanamume Akichagua Mke Wake*. Na mambo machache, hizo Jumbe, nataka kuzileta juma hili. Bali nataka tu kusanyiko . . .

136 Ambapo, kama kungekuwa na mhudumu hapa; mimi siko hapa, ndugu zanguni . . . Siwataki ninyi, ama baadhi ya wafuasi wenu, kurudi makanisani mwenu, na kusema, "Ndugu Branham alisema *hivi* na *vile*."

Mimi ninawajibika kwa Ujumbe ambao nimepewa na Mwenyezi Mungu. Kama ninavyosimama hapa usiku huu, na Mungu anajua hiyo ni kweli, ya kwamba papa hapa kwenye mto huu . . . Kuna watu, labda, wanaoketi hapa, wakati yule Malaika wa Mungu alishuka akaja pale na kuniambia aliyoniambia, pale pale katika mwaka wa 1933, moja kwa moja kwenye Barabara hii ya Spring hapa. Kama wewe ni mgeni hapa, telemka moja kwa moja. Ni pembeni mwa Barabara ya Spring, pale ambapo unafikia mtoni, hapo ndipo lilipotukia. Hiyo imekuwa katika mwaka wa 1933. Labda imekuwa yapata miaka thelathini na miwili iliyopita, basi. Loo, imekuwa thelathini na . . . imekuwa thelathini na . . . miaka thelathini na miwili iliyopita, miaka thelathini na miwili iliyopita.

Na jinsi ambavyo Yeye ameleta jambo hilo moja kwa moja, kila kitu. Nasi tumetoka, tukiuleta Ujumbe, na tukawaona wagonjwa wakiponywa, vipofu, na viwete, na vilema, na waliolemaa, na kila kitu. Halafu tukaona hata waliokufa, ambao tunajua imethibitishwa, wakifufuliwa katika wafu. Watu wanakufa, halafu wakafufuliwa tena, na mambo haya yote. Kama Ujumbe unatangazwa, kuna ishara na maajabu!

137 Na ungali unaona itikadi iyo hiyo ya kale uliyobuni? Hiyo haikutoka kwa Mungu. Mungu si lazima tu afanye ninino . . .

Mungu anajaribu kuufanya usikivu wako uvutwe kwenye Kitu fulani.

138 Ndipo wakati Yesu alipotoka akaenda, alianza kuwaponya wagonjwa, na kufanya kazi kubwa na kadhalika. Yeye, kila

mara, Yeye . . . Yesu alifanya hivyo. Na Musa na Yesu walifanya hivyo, na hao wengine. Na wakati alipokuwa hapa, Yeye alifanya hivyo.

Naye anafanya hivyo, jambo lile lile leo. Wakati Yeye anapopeleka mkutano kama huo, fufuo, na kuanza mkutano duniani, na kuanza kusonga mbele na ishara hizi kuu na maajabu. Halafu mnaona, mnairudia, itikadi iyo hiyo ya kale ya mafundisho, kuna—kuna kasoro mahali fulani hapo. Kuna kitu kipya kinachojitokeza! Wakati Yesu alipojitokeza, baada ya, wakati . . .

139 "Yeye ni rabi mzuri." Yeye angeweza kwenda katika mimbara yo yote na kuhubiri, wakati Yeye alipokuwa anawaponya wagonjwa. Wakati, loo, wao walipenda kuwa Naye kule.

Bali siku moja wakati alipoketi chini, na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," ndugu, Yeye hakupendwa na watu wengi baada ya jambo hilo. Wakati aliposema, "Msipoula mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu, hamna Uhai ndani yenu.

Bali Yeye aulaye mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele; nami nitamfufua katika siku ya mwisho." Basi, hakupendwa sana na watu wengi tangu wakati huo.

140 Wao walisema, "Mtu huyu ni kizuu kifyonza damu. Mtu huyu ni Beelizebuli. Hivyo ndivyo alivyofanya mambo hayo. Yeye aliweza kuagua. Yeye aliangalia katika nia za—zao na kujua mawazo yao. Yeye ni mpiga ramli."

Bali, jambo lilikuwa kwamba, Yeye—Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa kwa ajili ya wakati huo. Naye alikuwa na wajibu. Alisema, "Mimi daima hufanya kile kinachompendeza Baba Yangu." Mungu na atusaidie kufanya jambo lile lile, kufanya kile kinachompendeza Baba.

141 Nami natumainia nyote mtafahamu. Kama msipokubaliana nami katika Jumbe hizi na kadhalika, ya kwamba mtakumbuka, iweni ngaa na heshima hii lakini, ya kwamba mimi nina wajibu, nami siendi Tarshishi. Mimi niko njiani nikielekea Ninawi, nami si—sina budi kupiga kelele. Bwana na awabariki nyote.

Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

142 Ni karibu saa tatu u nusu. Sitaki kuwaweka, bali nataka kuona jambo hili kama nikiweza, usiku huu. Kuna wengine hapa ambao—ambao hamko hasa mahali mnapopaswa kuwa katika Kristo, bali m—mnataka kuwa, na mna hamu ya kuwa, hebu muinue mikono yenu, na kusema, "Ndugu Branham, niombee." Mungu akubariki, iangalieni tu hiyo mikono. "Na—nataka . . . Niko hapa, Ndugu Branham, kuwa karibu na Mungu."

Na kama kichwa chako kilikuwa kimeinuliwa, mkono wa—wangu umeinuliwa, pia. Hilo ndilo lililonileta hapa. Nina njaa, kama ninyi mlivyo nayo.

143 Lakini, loo, hivi majuzi, jambo moja la mambo mazuri sana lilitukia, nami sasa na—najua la kufanya. Nami na—naomba ya kwamba Mungu atawapa huo ufahamu dhahiri. Liko hapa. Lile. . . Kama kuna swali niani mwako, hapana budi pawe na jibu mahali fulani, kulijibu swali hilo. Maombi yangu, ni kwamba, Mungu awaruhusu kuona swali hilo likijibiwa mnamo wakati huu.

144 Kama u mgonjwa, Mungu na akuponye. Tutakuwa na ibada za kuponya, nafikiri, karibu kila usiku, nasi tutawaombea wagonjwa. Tutafanya kila tuwezacho kuwasaidieni, nanyi mfanye kila mwezacho kutusaidia. Nasi tutafanya kazi pamoja, tukitumainia ya kwamba Mungu atatupa mkutano mkuu.

145 Sasa, Baba Mungu, maneno haya machache yaliyokatwakatwa, bali wao wako mikononi Mwako sasa. Bwana, yamenenwa. Sina budi kukutana nayo. Kama tu vile. . . Maneno hayo hayawezi kufa kamwe; yanazungukazunguka dunia, kwenye rekodi, na siku moja sina budi kukutana nayo tena. Ninatambua jambo hili, Bwana, na nalisema kwa uaminifu mkuu sana.

146 Naomba, Mungu mpendwa, usiku huu, kwa ajili ya kila mmoja wa hawa, watoto Wako. Na, Ee Mungu, ninaamini, kabla ya juma hili kwisha, wao—wao watafahamu; ya kwamba swali, ambalo ni kuu sana niani mwao usiku huu, litatatuliwa. Tujalie, Bwana.

147 Kuna wengine hapa wasiokujua Wewe, Baba, kama Mwokozi, bado, ama labda hawajajazwa na Roho Mtakatifu. Naomba huu uwe ndio usiku huo.

148 Bwana, siwezi kumjaza mtu ye yote na Roho Mtakatifu; wala siwezi kumwokoa mtu ye yote. Ninaweza tu kuwaambia yale Wewe uliyosema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana hao watashibishwa." Nami naomba, Mungu, kwamba utasababisha njaa kama hiyo mioyoni mwao.

Wengi, Bwana, hapana shaka wana njaa; wangeendeshaje magari mamia haya ya maili, kupitia kwenye barafu na kila kitu, na kupanda milima yenye mvua, na kuvuka majangwa, kuja mahali padogo pa kale hapa pembeni! Kisha nafikiri tena, Wewe ulisema, "Palipo na Mzoga, tai wangekusanyika." Tulishe, Bwana, kwa Mana Yako ya Kiungu. Zipe nafsi zetu kile tunachohitaji. Tunakuonea kiu, Ewe Baba. Tuko mikononi Mwako sasa.

149 Naomba Roho Mtakatifu aliye mkuu aliyeshuka kwenye ule mlima juzijuzi kule juu, naomba ya kwamba ataujaza kabisa kila moyo ulio hapa ndani na wema Wake pamoja na rehema, na ufahamu. Tunatambua, Baba, hilo ndilo tunalohitaji, ni kufahamu. Kwa kuwa kama hatujui tunalofanya, basi tunajuaje jinsi ya kulifanya? Bali hatuna budi kuwa na ufahamu. Kama alivyosema Danieli, yeye alipata "kufahamu kwa njia ya

Maandiko ya Yeremia." Basi, Baba, tunafahamu kwa njia ya Maandiko ya Roho Mtakatifu, kama atakavyotufunulia katika saa hii. Tupe, Bwana, shauku tuliyo nayo kwa ajili Yako. Tunaomba jambo hili kwa unyenyekevu, Baba, kwa Utukufu Wako, katika Jina la Yesu Kristo.

150 Sasa vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa. Wakati dada yetu anapiga kinanda, basi, "Yeye atanipa neema na utukufu, na kuambatana na mimi kote." Nawatakeni sasa muombe tu kimya-kimya na kumwomba Baba wa Mbinguni ya kwamba atawajalia, usiku wa leo, mahitaji yenu.

151 Ndugu mpendwa, dada mpendwa, Yeye yu karibu tu kama vile mkono wako ulivyo kwako. Ninyi, mmeniamini mimi katika—katika mambo mengine, niaminini katika jambo hili. Yeye yuko hapa kuwapa cho chote mnachohitaji.

152 Loo, kwa majuma machache yaliyopita nimekuwa na njaa sana, na kiu sana, nikitamani kwenda nyumbani sana, kuwaona ninyi. Hiyo ndiyo sababu nilisema, "Billy, twende nyumbani."

Meda akasema, "Kwa nini unataka kurudi kule, kwenye hiyo nchi yenye baridi tena, Bill? Sikuzote unashikwa na mafua na kila kitu. Sikuzote unatoka huko, kichwa baridi, na umepwelewa na sauti, na ni vigumu kwako kuzungumza."

153 Nikasema, "Vema, sijui." Nikamwambia . . . Naona rafiki yangu, Charlie Cox, ameketi kule nyuma. Nikasema, "Mimi nina hamu tu ya kumsikia Charlie akisema, 'Maskini kindi yule lipanda mti ule kule.' Ninatamani sana kusikia hayo." Na—nataka tu kuwa—kuwa karibu nanyi.

154 Najua Ndugu yangu Banks alikuwa mgonjwa sana. Nami niliona ono lake, hapa si muda mrefu uliopita, naye alikuwa amelala kichalichali. Nami najua alikaribia sana kutuacha, hivi majuzi. Ninapowaangalia ninyi wengine . . .

155 Nilikuja usiku wa juzijuzi, kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara Wakristo, na wa mataifa yote. Mzee "Baba" Shakarian, babaye Demos, alizoea kuketi pale na akaendelea kuangalia hata nilipoingia, kisha angetabasamu, na huko kunipungia mkono kidogo angalinipungia mimi. Yeye hakuweko. Amekwisha kuaga dunia.

Ndipo nikaja kwa jamaa hiyo, nikiwa na BWANA ASEMA HIVI, binti yao atakufa, pia. Florence, nilimwona katika ono, nikamwona akiaga dunia. Nami najua ataaga dunia. Nami nikasema, "Ombeni, ombeni tu. Mnajua kuna . . . Nabii fulani wakati mmoja aliambiwa aende akamwambie mfalme fulani aweke nyumba yake katika utaratibu. Naye akaomba, na maisha yake yakahifadhiwa, miaka kumi na mitano zaidi." Nikasema, "Ombeni."

156 Lakini, angalia, nami ni—nikarudi. . . Niliketi hapa mkahawani, juzijuzi, nikila. Mtu fulani akanijia, kasema, “Hivi wewe si Billy Branham?”

Nikasema “Naam.”

157 Labda hakunijua, sababu ya sehemu *hii* yenye upara kichwani mwangu. Nilikuwa nikivaa kipande hiki cha nywele, nisije nikapata mafua kwenye mkutano huu.

Naye akanijia, akasema, “Nilifikiri nilikujua, Billy.”

Nikasema, “Naam.” Nikasema, “Wewe ni nani?”

Kasema, “Mimi ni John Warman.”

Nikasema, “Habari za Zip?”

Akasema, “Billy, alikufa.” Mhu!

158 Nilikuwa nikishuka kuja kwenye jumba la mahakama; nikashuka nikaenda kulipa kodi zangu. Nilipokuwa ninashuka kupitia hilo jumba la mahakama, bibi fulani akanipigia kelele, akasema, “Hivi ulijua John ameaga dunia?” Ama, jina fulani. Huenda ikawa haikuwa John; Ed, ama kitu fulani. Nami nikasema. . . Sikumjua huyo mwanamke. Nikatahayari. Ndipo nikapata kujua, mimi sikujua alikuwa ni nani.

Akasema, “Unakumbuka usiku mmoja wenye giza wakati mto ulikuwa umefurika kwenye zile kingo nje hapa, na nyumba zilikuwa zinapelekwa na maji, huko kwenye barabara ya Chestnut, nawe ukayahatarisha maisha yako kwenda mahali fulani ukamtoe mwanamke fulani na watoto wadogo wachache?”

Nikasema, “Wewe ndiye?”

159 Naye akasema, “Mimi—mimi ndiye huyo bibi.” Alianza kupiga mayowe kwa ajili ya mtoto wake mchanga; mnajua hadithi yangu. Yeye akasema, “Huyo niliyemwita ‘mtoto wangu mchanga,’ ameolewa na ana jamaa.” Mnaona? Na ndiye huyu hapa, mzee na mwenye mvi; nami ndiye huyu hapa, pia.

160 Mmoja mmoja, kadi zetu zinatolewa kwenye rafu, kama ilivyokuwa. Nasi tunafanya mikutano, nami ninamkosa huyu, ninamkosa *yule*. Sisi sote hatuna budi kukosekana, moja ya siku hizi.

Lakini, ndugu, dada, kuna Mahali pa kukutanika. Hebu na tuhakikishe ya kwamba tuko sawa. Sivyo? Usiache ufahamu wetu wote wa Mungu, na kadhalika, uende bure. Na tuamini.

161 Baba, wako mikononi Mwako. Mimi niko mikononi Mwako, Bwana. Tuko tu hapa kwa kujiweka wakfu sasa, kabla ya mkutano unaokuja unaoanza kesho usiku. Utatusaidia, Bwana? Ma—mazungumzo yetu na yawe daima juu Yako! Mioyo yetu na nia zetu na ziwe juu Yako Daima, nawe ulisema ungetuweka katika amani kamilifu. Pia imeandikwa katika Biblia, “Usizitegemee akili zako.” Ee Mungu, hatutaki akili zetu;

tunataka akili Zako. Tupe hizo, Ee Mungu. Ufufuo na uje nafsini mwetu hata kundi hili la watu litakuwa tu katika moyo mmoja na nia moja. Tujalie, Baba. Tujalie mambo haya, tunapoomba katika Jina la Yesu Kristo.

Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

Msalaba, masalaba,
Humu ni-. . .(hebu tuinue mikono yenu). . .
sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

Yesu unihifadhi
Hapa Msalabani
Wajiao. . .(ndiyo, Bwana, huru). . .Kalvari,
Waponywe damuni.

Msalaba, msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

162 [Ndugu Branham anaanza kuuvumisha *Karibu Na Msalaba*—Mh.] Ee Mungu! Kama kuna mmoja wenu anayejisikia kwamba angetaka kuja na kupiga magoti madhabahuni, kama ukitaka kuja, useme, "Mimi siko ninakopaswa kuwa, Bwana. Mimi—mimi nataka kujiweka wakfu tena. Nataka kufanya hivyo usiku wa leo, Bwana." Unakaribishwa kuja. Tutakuwa hapa kuomba pamoja nawe. [Ndugu Branham anaendelea kuuvumishaa *Karibu Na Msalaba*.]

Msalaba, msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

Yesu unihifadhi,
Hapa Msalabani;
Wajiao Kalvari,
Waponywe damuni.

Msalaba, msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

163 Hebu na tuombe tu, kila mmoja katika njia yako mwenyewe sasa. Sa—sahau tu wakati. Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu katika Uwepo Wake. Maskini bibi huyu hapa, anayepaza sauti, "Nakupenda Yesu!" Mnakumbuka mlipookoka, miaka mingi iliyopita, unakumbuka jinsi jambo hilo lilivyokuwa tamu kwako? Yeye yungali mtamu namna hiyo usiku wa leo. Na

tuombe, kila mtu kwa njia yake sasa. Hebu tu—hebu tu tujiweke wakfu kwa Mungu, tujiweke wakfu tu kwa Bwana.

164 Mpendwa Bwana Yesu . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

> Kijito cha faraja zangu zote,
> Ni zaidi ya uhai kwangu;
> Nina nani duniani ila Wewe?
> Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?.

Mungu mpendwa, tunaomba sasa ya kwamba rehema yako na neema itatumwa juu ya kila mmoja wetu, Bwana. Tuko hapa tumeyazunguka madhabahu. Wengi hawangeweza kuja humu; Wewe utakutana nao kwenye viti vyao. Cho chote tunachotoa, Bwana, Wewe uko tayari kupokea. Kama tu tukikutolea wakati wetu, utaupokea; majaliwa, utayapokea. Bali, Bwana Mungu, usiku wa leo tunaenda zaidi ya hapo, tunakutolea yote tuliyo sisi. Yote niliyo mimi, yote ninayotarajia kuwa, yote yako ndani yako, Bwana. Tunaomba ya kwamba utachukua haya, maombi yetu, uyaweke moyoni Mwako, Bwana, na utupe kina kirefu cha Roho Mtakatifu, maisha yetu yapate kubadilishwa. Kwa maana, tunaona ya kwamba tuko karibu na mwisho sasa. Haiwezi kuwa wakati mwingi zaidi. Na tunapowaona wapenzi wetu wakianguka, siku baada ya siku, vijana kwa wazee, tunajua hivi karibuni hayana budi kupiga hodi mlangoni mwetu. Na usiku wa leo, Bwana, wakati tungali tuna akili timamu, tukiketi hapa, ama kupiga magoti hapa, kusimama hapa, mahali po pote tulipo, tupokee, Bwana Mungu.

165 Nitwae, Bwana. Mimi si kitu, bali hata niwe nini, Bwana, kama unaweza kunitumia kwa njia yo yote, ninajiweka wakfu Kwako.

166 Naomba, Mungu Mpendwa, kwa ajili ya kila mmoja wa hawa. Watu hawa wapendwa ambao nilisimama kule kwenye milima ya Arizona na kulia kwa ajili yao, na hawa hapa wamepiga magoti pamoja nasi madhabahuni usiku wa leo, tukiomba, tukiyaweka maisha yetu wakfu. Tunakupenda, Baba, kuliko maisha yetu wenyewe. Tunakupenda kuliko jamaa zetu. Tunakupenda kuliko mke, watoto, baba, mama, dada, ndugu, mume, mke. Tunakupenda, Bwana Yesu. Fanya jambo hilo liwe halisi sana mioyoni mwetu, Bwana. Mwaga mafuta ya furaha, juma hili, Bwana, ndani ya nafsi zetu. Tupe kuoshwa, kuoshwa kwa Neno, kwa maji ya Neno, ukitugawia Kweli.

167 Wengi hapa usiku wa leo, Bwana, na watakuwa hapa, ambao wametatanishwa na masomo haya ambayo ni muhimu sana. Ee Mungu, fungua chemchemi hiyo katika nyumba ya Mungu, ambayo ni—ni ya kutusafisha sisi. Naomba, Mungu, ya kwamba utatuosha na kutusafisha, katika Damu Yako, na utufanye viumbe vipya. Pia tupe neema na nguvu, kulileta Neno la Kweli katika ufunuo Wake wa Kiungu wa Utu wa Yesu Kristo.

Naomba kwamba atokee mbele zetu, Bwana. Naomba aje ayaponye maradhi yetu, azisamehe dhambi zetu, aijaze mioyo yetu yenye njaa na habari njema ya furaha kuu, Injili iliyodhihirishwa maishani mwetu.

Mbariki kila mchungaji, kila kiongozi wa nyimbo, kila mwalimu wa shule ya Jumapili. Tubariki sote, pamoja, Bwana, kwa maana kweli tunakupenda. Na sasa sisi tu Wako, Bwana, katika huku kuwekwa wakfu. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tutumie sasa kulingana na mapenzi Yako Mwenyewe.

Yesu kwa imani,
Nakutumaini,
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni Wako kabisa
Tangu leo!

Mnaupenda huo? Hebu tuuimbe tena.

Hapa nazunguka
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza
Utaniongoza
Hivi nitaweza
Kufuata.

Huo unawafanya mjisikie vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanapenda kuziimba hizo nyimbo za kale? ["Amina."] Mimi nazipenda sana. Nanyi je?

Lo, twenenda Sayuni,
Mji mzuri Sayuni;
Twenenda juu Sayuni,
Ni maskani ya Mungu.

Loo, twenenda Sayuni,
Loo, Mji mzuri Sayuni;
Twenenda juu Sayuni,
Ni maskani ya Mungu.

Mpendao Bwana
Ije raha yenu!
Imbeni nyimbo za raha
Imbeni nyimbo za raha
Wa ibada yenu
Wa ibada . . .

Sasa, hebu tusimame sasa tunapouimba. Peaneni mikono ninyi kwa ninyi.

Twendeni Sayuni,

Akubariki, dada! Akubariki, dada! Akubariki, ndugu! Akubariki, dada! [Ndugu Branham anaendelea kuwasalimu watu—Mh.]

Ni maskani ya Mungu.

Na tumwinulie Mungu mikono yetu sasa.

Lo, twenenda Sayuni,
Mji mzuri Sayuni;
Twenenda juu Sayuni,
Ni maskani ya Mungu.

Loo, twenenda Sayuni,
Loo, Mji mzuri Sayuni;
Twenenda juu Sayuni,
Ni maskani ya Mungu.

Huo hauwafanyi mjisikie vizuri sana? [Kusanyiko linafurahi—Mh.] Jamani, jamani! Loo, hebu na tuinue mikono yetu na tumsifu tu Yeye katika njia zetu wenyewe.

168 Bwana Yesu, Wewe uliye Waridi wa Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, Nyota ya Asubuhi Inayong'aa, Aliye Mwema kuliko elfu kumi nafsini mwangu. Wewe uliye kijito cha faraja yangu, uliye zaidi ya maisha kwangu mimi! Jinsi tunavyokupenda! Tusikie sasa, Bwana. Jinsi tunavyokushukuru Wewe! Loo! [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] Jinsi tunavyokushukuru! Wabariki hawa, Bwana na Mwokozi wangu wa thamani! Tujalie mambo haya, Bwana. Tujalie. [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanaendelea kuomba na kumsifu Mungu—Mh.]

Msalaba, msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

169 Kwa njia fulani, ama nyingine, najisikia tu tutaninino... Kuna kitu fulani kilicho moja kwa moja mbele zetu. Sasa, kumbukeni tu, ninaamini ninatabiri. Furaha kuu iko mbele yetu. Aminini hilo. Hiyo ni kweli. Mioyo mingi yenye huzuni itafanywa... Siri kuu zitafanywa wazi, na watu walio na huzuni watapata furaha. [Kusanyiko linafurahi—Mh.]

Msalaba, Msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika,
Mahali pa raha.

170 Kama vile Yohana wa kale, wakati alipokuwa mzee sana asiweze kuhubiri, yeye angeketi tu na kupaza sauti, ndivyo wanavyoniambia, na nguvu zake zote, "Enyi watoto wadogo, pendaneni!" Pendaneni. Msiache kitu kije miongoni mwenu, mnaona. Wekeni kando, kila kitu mbali na... Naam, hata iwe nini, kikabilieni. Tunaenda zetu Ninawi. Mnaona? Msiingie kwenye hiyo meli ya Tarshishi, ambayo inawatoa ninyi kwenye

hili kundi. Hebu na twendeni moja kwa moja kwenye kijito cha baraka za Mungu. Ninaamini tutazipata. Namwamini Baba yetu.

171 Unajisikia vizuri sasa, dada? Hilo ni sawa. Hivyo ndivyo ninavyotaka kuwaona watoto wakizaliwa, wakija namna hiyo. [Yule dada anaendelea kuomba na kufurahi—Mh.]

Naweza tu kufikiria juu ya miaka mingi iliyopita, papa hapa kwenye ardhi hii, ni maelfu wangapi wamezaliwa katika Ufalme wa Mungu, papa hapa kwenye ardhi hii. Jinsi hatukujua mengi, tulipokuwa tukisimama hapa na senti themanini mfukoni mwetu, kulijenga kanisa hili kwazo! Loo, Yeye alisema, "Mimi Bwana nimelipanda, nitalinyunyizia maji usiku na mchana." Naye amefanya hivyo. Amefanya hivyo.

Mungu awabariki. Sasa wakati tunapoviinamisha vichwa vyetu . . .

172 Sasa, kesho usiku, kumbukeni, ibada zitafanyiwa huko kwenye ukumbi wa hii shule hapa. Na kama . . . Tutamweka mtu hapa sasa, kuwaonyesha watu namna ya kwenda kule, kwa maana wageni watakuja.

173 Mnampenda, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."]

174 Nilikuwa nimesimama hapa chini ukingoni, na kuimba ule wimbo wa kale:

> Nasimama ukingoni wenye dhoruba wa Yordani,

Wazia, hiyo imekuwa miaka thelathini iliyopita, thelathini na mitatu, miaka thelathini na mitatu iliyopita.

> Na kuangalia kwa shauku,
> Nchi ya Kanani nzuri na ya furaha,
> Ilipo mali yangu.

Na wengi niliowabatiza, jioni hiyo, wako kule ng'ambo sasa. Ambapo, walisimama pale na kushuhudia hiyo Nyota ya Asubuhi ikishuka kuja kutoka mbinguni, ikizungukazunguka namna hiyo, kasema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kuleta, kutangulia kuja kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia kule Kuja kwa pili." Ingewaziwaje? Bali, Maneno yote ya Mungu ni ya kweli, Maneno yote ya Mungu. Tunaishi kwenye Uwepo wa yule Mfalme mkuu. Mungu awabariki.

175 Tunapoviinamisha vichwa vyetu, nitamwomba Ndugu Neville, mchungaji wetu wa thamani, aje hapa aturuhusu tufumukane kwa maombi. Mungu akubariki, Ndugu Neville.

Mtu Anayejiepusha Na Uso Wa Bwana SWA65-0217
(A Man Running From The Presence Of The Lord)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano, tarehe 17 Februari, 1965 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org